epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Ijumaa Aprili 19, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581651
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



**'KIPIGO HAKIJAHARIBU MSIMU WETU'** UKURASA 22

UKURASA WA 3

### BITEKO: BWAWA LA UMEME LA JULIUS NYERERE LI SALAMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amesema licha ya mvua zinazoendelea...

UKURASA WA 4

### SAMIA AJIVUNIA KUPAA BIASHARA TANZANIA, UTURUKI

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema Tanzania na Uturuki, zimeshuhudia ongezeko la...

UKURASA WA 5

### KESI MATUNZO WATOTO ZAZIDI KUSHIKA KASI

KATI ya mashauri 14,600 yaliyoshughulikiwa ya migogoro ya ndoa yaliyohusu masuala ya kifamilia...



# Kemikali za kilimo zachangia ongezeko saratani

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akitunukiwa Shahada ya Heshima ya Udaktari (Honoris Causa) ya Uchumi kutoka kwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ankara nchini Uturuki, Prof. Necdet Unuvar kwenye hafla iliyofanyika Chuoni hapo jana. **PICHA: IKULU**

## Sheria ya makosa dhidi ya ukatili mbioni kufumuliwa

UKURASA 3

# Kikokotoo, ripoti ya CAG, Katiba kutawala maandamano CHADEMA

• **Kinana** ataka majibu sahihi, Mbunge ataka kiwaguse na wao pia... *Endelea ukurasa 2*





Wanawake wa Kimaasai kutoka jamii ya wafugaji wa kijiji cha Nanja, wilayani Monduli, mkoani Arusha wakimwaga maziwa kama ishara ya ibada ya kuliombea Bwawa la Asili la Nanja jana, lililoanza kutoweka baada ya kumeguka kingo zake na kusababisha upotevu wa maji yaliyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na mifugo. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Kemikali kilimo zachochea saratani

**Na Restuta James**

WANAHARAKATI wa haki za binadamu wamesema matumizi yasiyo sahihi ya kemikali kwenye kilimo, yanachangia ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza kama kisukari, saratani, figo na moyo.

Kutokana na hali hiyo, wanaharakati hao wameanzisha utafiti ili kubaini ni kwa kiwango gani viuatilifu hivyo vinahatarisha afya za wananchi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Tanzania Relief Initiative (TRI), Wakili Edwin Mugambila, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa takwimu za kimataifa zinaonyesha kuwa asilimia 70 ya vifo vinavyotokana na magonjwa yasiyoambukiza vinawapata watu kabla ya wakati.

"Moja ya visababishi vikubwa vya NCD ni ulaji usiofaa. Tumekuwa mara kwa mara tukizungumzia matumizi ya sukari, chumvi, mafuta, pombe na tumbaku kama kichochezi lakini kuna tatizo kubwa ambalo ni kemikali zitokanazo na viuatilifu katika kilimo cha kisasa.

"WHO (Shirika la Afya Duniani) inasema hizi kemikali zinazotumika kwenye kilimo zinasababisha asilimia 25 ya vifo vyote vinavyotokea duniani kila mwaka yanayotokana na maradhi ya moyo, figo, saratani na kisukari. Njia hatari zaidi ni kemikali kuingia kwenye damu kwa kula vyakula vilivyolimwa kwa viuatilifu hatarishi.

"Unaweza kusema mimi situmii chumvi, sukari, mafuta, sinywi pombe wala sivuti sigara lakini utanunua nyama, karoti, kitunguu, mchicha au embe ambalo limelimwa kwa kemikali mbaya sana. Wataalamu wanasisitiza tule mboga na matunda na lishe bora lakini kwa sasa hii ni hatari kuliko sukari,' alisema.

Alisema baadhi ya kemikali zilizoko kwenye viuatilifu ni 'carbosulfan' inayotumika kudhibiti visumbufu kama wadudu wakiwamo mchwa, minyoo kwenye viazi, mpunga, mahindi na baadhi ya matunda.

Alitaja kemikali nyingine kuwa ni 'diazinon' inayotumika kuua mende, mchwa na jamii ya nzi kwenye majengo. Nyingine ni DDT ambayo ilipigwa marufuku baada ya kutumika kwa miongo mingi na kubainika kusababisha maradhi ya saratani. DDT pia inatumika kuangamiza mazalia ya mbu nchini.

Kemikali nyingine, alisema ni 'endrin' inayotumika kudhibiti visumbufu vya mazao kama panya na ndege waharibifu.

"Utafiti wa kitaalamu unatuambia kwamba kemikali hizi zinahusishwa kusababisha magonjwa kama saratani ya tezi dume, maini na damu, magonjwa ya moyo, ya sukari, ugonjwa wa kutetemeka, figo, kuzeeka na upumuaji.

"Haya ni matatizo makubwa sana ambayo yanasababishwa na matumizi ya kemikali." alisema.

**MZIGO MKUBWA**

Kwa mujibu wa Mugambila, Tanzania inatumia zaidi ya Sh. bilioni 99 kila mwaka kutibu magonjwa yasiyoambukiza na kwamba asilimia 13.2 ya vifo nchini vinatokana na maradhi hayo.

Alisema hivi karibuni, Malaysia ilifanya utafiti na kubaini kwamba miaka michache ijayo, asilimia 72 ya wakulima waliokuwa wanatumia viuatilifu vyenye kemikali hizo, watapata maradhi ya saratani na moyo na kwamba matumizi ya kemikali yana madhara makubwa kwa siku zijazo.

Pia alisema takwimu za kimataifa zinaonyesha kwamba kila mwaka watu milioni moja hufariki dunia kwa magonjwa yasiyoambukiza duniani ambao asilimia 70 kati yao wanafariki kabla ya wakati.

"Asilimia 17.9 ya watu hufariki (dunia) kwa magonjwa ya moyo kila mwaka, asilimia tisa kwa saratani, asilimia 3.9 magonjwa ya upumuaji na asilimia 1.6 kwa kisukari," alisema.

# Kikokotoo, ripoti ya CAG, kutawala maandamano CHADEMA

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na Makamu Mwenyekiti wake, Tundu Lissu, wamepanga kutawanyika katika mikoa 14 kuendesha awamu nyingine ya maandamano kuanzia Aprili 22 hadi 30, mwaka huu, huku ajenda ya kikokotoo ikitawala maandamano hayo.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alisema mikoa ambayo viongozi hao wataongoza maandamano hayo ni Kanda ya Serengeti yenye mikoa ya Shinyanga, Mara na Simiyu.

Mingine ni Kanda ya Victoria yenye mikoa ya Kagera, Geita na Mwanza na Kanda ya Kaskazini yenye mikoa ya Arusha, Tanga, Manyara na Kilimanjaro. Pia alisema watakwenda Kanda ya Kati yenye mikoa ya Singida, Dodoma na Morogoro.

Alitaja baadhi ya ajenda zitakaongoza maandamano hayo ni pamoja na Kikokotoo cha mafao ya wastaafu, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali(CAG), Katiba mpya na athari za mvua.

"Kwa hiyo awamu ya kwanza itakayoanza Aprili 22, tutaanzia kanda hizo nne na viongozi wakuu wa chama wataongoza maandamano hayo," alisema Mrema.

Alisema Aprili 22, Mbowe ataongoza maandamano Bukoba na siku inayofuata atakwenda Kahama mkoa wa Shinyanga kisha Aprili 24 Geita mjini na 25 Bariadi na baadaye Musoma mjini Aprili 26.

Alisema Aprili 27 ataongoza maandamano Mwanza wilaya ya Sengerema, Aprili 29 ataongoza maandamano mkoa wa Tanga na Aprili 30 mkoa wa Kilimanjaro.

Kuhusu Makamu Mwenyekiti Lissu, alisema ataanzia Kanda ya Kaskazini Aprili 25 mkoani Arusha, Aprili 26 Manyara siku inayofuata 27 Singida mjini kisha Aprili 29 Dodoma mjini na kumalizia Morogoro Aprili 30.

Kwa mujibu wa Mrema, mbali na mikoa hiyo, huenda wakagusa na mkoa wa Katavi katika awamu hiyo kutokana na maandalizi ambayo yamefanywa kwenye mkoa huo.

"Kwa hiyo tutakuwa na misafara miwili na tumeshalijulisha Jeshi la Polisi katika maeneo hayo kutakakofanyika maandamano,"alisema Mrema.

Akizungumzia msimamo wa CHADEMA kuhusu kikokotoo, Mrema alisema wanachotaka ni serikali kutumia utaratibu wa zamani wa kuwalipa wastaafu mafao yao yote na kuachama na kanuni ya asilimi 33 wanayoitumia katika kikokotoo kipya.

"Msimamo wetu kuhusu kikokotoo ni kwamba, fomula ya waliyotumia ya kuwalipa wastaafu asilimia 33 ya mafao yao ni mbaya kwa sababu inawaumiza,"alisema Mrema.

"Wako wastaafu ambao tunafahamu wanakaa kwenye makambi na hawa ni askari polisi, wanajeshi ambao unapompatia hiyo asilimia 33, hajajenga hata kibanda kwake na alitegemea mafao hayo ndio akajenge, leo ukimpatia hiyo hawezi kujenga na anaondolewa kambini," alisema.

Mrema alisema ni vyema wastaafu wakapewa mafao yao yote badala ya kuwapatia kidogokidogo.

"Hizo ni fedha za mfanyakazi ambazo aliwekeza kidogokidogo kwa kukatwa kwenye mshahara wake, kwa nini wakati wa kutumia serikali impangie, eti inasema ukiwapa zote zinaisha haraka, kwani wamekuja kukulalamikia kwamba zimeisha, wapeni haki yao kama ilivyokuwa kabla ya hiki kikokotoo kipya," alisema Mrema.

# Kinana ataka majibu sahihi

**Na Maulid Mmbaga**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Bara Abdulrahman Kinana amesema kutokana na malalamiko dhidi ya kikokotoo kuendelea kuongezeka nchi nzima, wataenda kulijadili kwenye vikao vikuu vya chama na lazima watoke na majibu sahihi.

Kinana aliyasema hayo jana wakati akijibu swali liloulizwa na Mwalimu wa Shule ya Msingi Silanga A, Wilaya ya Musoma Vijijini, Nyakusanya Mkangara aliyetaka chama hicho kuishauri serikali ilegeze msimamo wake kwakuwa kikokotoo si rafiki na kinaenda kuwaumiza wastaafu.

Alisema kama serikali haijapata suluhu ya malalamiko yao basi kikokotoo hicho kianze kutumika kwa walimu walioanza kuajiriwa kuanzia mwaka 2018 ilipoanzishwa sheria hiyo na walimu wa nyuma ya mwaka huo waendelee kutumia sheria ya zamani.

Kutokana na kuwasilishwa hoja hiyo iliyoulizwa kwenye mkutano wa ndani, Kinana katika majibu yake alisema.

"Suala la kikokotoo litafikishwa kwenye vikao vikubwa vya chama, litajadiliwa kwasababu limepigiwa kelele na hatuwezi kujidai hatujui, hatujasikia na hatuna habari, malalamiko yapo na yanaendelea kuongezeka, tutalijadili vizuri kuona njia nzuri inayofaa na lazima tuwe na majibu sahihi," alisema Kinana mara baada ya kupokea malalamiko ya mwalimu na mbunge.

Awali, Mwalimu Makaranga alisema amekuwa akipata simu nyingi kutoka kwa walimu wanaokaribia kustaafu na waliokwisha staafu wakilalamikia kikokotoo, wakieleza kwamba asilimia 33 ni fedha ambayo haiwatoshelezi kutokana na mahitaji yao.

"Kwasababu fedha hiyo ni ndogo tunaomba angalau tupewe asilimia 50, au kiwakumbe wale walioanza kufundisha mwaka 2018, sisi tulioajiriwa miaka ya 70 kisituguse," alisema na kuongeza:

"Tunashauri hivyo kwasababu mpaka wanakuja kustaafu thamani ya shilingi itakuwa imependa, hata wakipiga asilimia 33 watakuta hela iko nzuri, lakini kwetu tulioanza miaka ya nyuma thamani ya hela imeshashuka na mahitaji ni mengi, inatuumiza," alisema Mkangara.

Aidha, alieleza kuwa asilimia hiyo ni ndogo ikilinganishwa na kiwango cha mahitaji yao huku akieleza kuna wanaostaafu hawana nyumba na wamekuwa wakisomesha watoto shule binafsi.

Mbunge wa Musoma Mjini (CCM), Vedastus Matayo, alisema alipokea malalamiko ya walimu wakimuomba awasemee kwakuwa wanapostaafu wanaenda kujiandaa na maisha hivyo wanashauri wapatiwe asilimia 50 ya kuendesha maisha kwasababu hiyo kidogo kigodo inawafanya waelemewe na majukumu mengi.

"Wakipatiwa hiyo kidogo kidogo mwingine ndani ya miaka mitano anapoteza maisha kwasababu ya msongo wa mawazo 'stress', kwahiyo nimelipokea na nadhani nitalifikisha kwa Rais Samia Suluhu Hassan, ili tatizo hilo liishe," alisema Matayo.

## HABARI KITAIFA

# Sheria ya ukatili kufumuliwa

**Na Vitus Audax,** DODOMA

SERIKALI imesema ipo tayari kufanya mapitio ya sheria zinazohusiana na vitendo vya ukatili, ukiwamo wa kijinsia, ambavyo vimeendelea kukithiri nchini ili wahusika wachukuliwe hatua kali za kisheria na hatimaye kuvikomesha.

Akijibu maswali ya papo kwa papo kutoka kwa wabunge jana, alisema serikali inatambua kukithiri kwa vitendo hivyo, hususani ukatili wa kijinsia, katika baadhi ya maeneo nchini na kwamba suala hilo liko chini ya wizara mbalimbali na hatua zimekuwa zikiendelea kuchukuliwa.

Akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Tunza Malapo, aliyetaka kujua mkakati wa serikali kudhibiti vitendo hivyo, alisema: "Kwa kuwa nimekiri kwamba tatizo hili lipo kwa baadhi ya maeneo nchini na hatua kali zinachukuliwa, lakini yanajirudia kutokana na sheria zake kuwa si kali sana, jambo hili ni mtambuka na linagusa wizara nyingi na kila wizara inaweka sheria yake katika kukinga jambo hili.

"Kwahiyo tunapokea ushauri wa kufanya mapitio kwa sheria hizi malengo yetu yakiwa kuhakikisha jamii inakuwa salama na wale wote wanaoendelea kufanya matendo haya wanachukuliwa sheria kali. Tunatamani tuone jambo hili likikoma kwenye jamii."

Aidha, Waziri Mkuu aliitaka jamii kuzingatia mila na desturi njema ili kuepuka kutumbukia katika matendo kama hayo ya kikatili kwa kuwa kila mtu ana haki ya kuishi.

"Kwanza tupunguze ulevi holela unaosababisha watu kutenda mambo kinyume cha akili zao, imani na mila potofu pamoja na malezi ambavyo vimekuwa chanzo cha matukio hayo. Pale panapohitajika mabadiliko ya sheria na kanuni, tuko tayari kuileta hapa bungeni ili kuzibana zaidi," alisisitiza.

Awali, Malapo alisema matukio ya unyanyasaji wa kijinsia kwa watoto, wanawake, makundi mengine pamoja na wanyama, yamekithiri nchini licha ya adhabu mbalimbali kutolewa, hivyo kuitaka serikali kuweka muswada mezani kwa ajili ya kuongeza au kubadili adhabu zinazotolewa ili zikidhi haja ya kukomesha matukio hayo.

### LESENI ZA MADINI

Waziri Mkuu alisema serikali ina nia ya kuyatwaa maeneo yote makubwa ya madini yanayomilikiwa na wawekezaji, bila kufanya kazi yoyote na kuyagawa kwa wachimbaji wadogo ili kuwasaidia kupata fursa ya kuchimba madini.

Alisema hayo wakati akijibu swali la Mbunge wa Kishapu (CCM) Boniface Butondo, aliyetaka kupata ufafanuzi kuhusu kauli ya serikali kudhibiti ongezeko la leseni zinazohodhi maeneo makubwa bila kufanyiwa kazi na kuwanyima fursa wachimbaji wadogo wanaohitaji maeneo hayo.

"Wako wanaomiliki maeneo makubwa ya madini lakini hakuna kazi yoyote inayofanyika kwenye maeneo hayo na wengine hawajalipia gharama za kutenda na kutekeleza shughuli hizo. Lakini waziri alishatoa maelekezo hapa kwa wakuu wa mikoa kufanya mapitio na kutwaa maeneo hayo," alisema Majaliwa.

Pia aliwaagiza makamishna wa madini na mameneja wa mikoa kukamilisha kazi hiyo kwa wakati ili serikali ifute leseni hizo na kuanza kuyagawa kwa wachimbaji wadogo.

### MICHANGO YA MAAFA

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu aliwaagiza wakuu wa mikoa na wilaya ambao pia ni wenyeviti wa kamati za maafa katika maeneo husika kutekeleza wajibu wao wa kutoa mrejesho wa michango na misaada inayotolewa na wadau mbalimbali katika kukabiliana na maafa yanayotokea.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuweka uwazi na imani kwa jamii na wadau ili waendelee kuhamasika kutoa michango zaidi, ili kuzisaidia jamii zinazopatwa na maafa pamoja na urejeshaji wa miundombinu.

# Biteko: Bwawa la umeme Julius Nyerere liko salama

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amesema licha ya mvua zinazoendelea kunyesha nchini, Bwala la Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) lipo salama kutokana na kujengwa kisayansi na kuendelea kuzalisha umeme kupitia mtambo namba tisa huku mitambo mingine miwili ikiwa ukingoni kukamilika.

Alisema jana jijini Dodoma katika mahojiano kuhusu Maonesho ya Wiki ya Nishati 2024, yanayoendelea katika viwanja vya Bunge.

"Bwawa letu lipo salama kwani limejengwa kisayansi, ujazo wake wa maji ni mita za ujazo 183 na kwa takwimu za leo (jana) ni mita za ujazo 183.4, huko nyuma maji yalikuwa yakiingia mengi sana kwa kiasi cha mita za ujazo 8,400 kwa sekunde hivyo yalipaswa kupunguzwa ili kuendana na ujazo wa bwawa," alisema Dk. Biteko.

Alisema, bila ya kuwapo kwa bwawa hilo athari za mvua zingeanza kuonekana tangu mwezi Oktoba, mwaka jana, lakini hali hiyo haikutokea mapema kwa sababu maji yalikuwa yakijazwa katika bwawa kwa ajili ya kuzalisha umeme.

Aidha, Wizara ya Nishati na TANESCO ilishabaini uongezekaji wa maji katika Mto Rufiji, kuanzia mwezi Februari, mwaka huu na tahadhari ilianza kutolewa kuhusu kasi hiyo ya maji ili kuanza kuchukua hatua stahiki. Dk. Biteko ameeleza kusikitishwa na athari zilizotokea kutokana na mafuriko ambayo yamesababisha maisha ya watu na mali zao na kuwa serikali inafanya kila jitihada kurejesha hali ya kawaida kwa wananchi waliokumbwa na maafa hayo.

Kuhusu utekelezaji wa ajenda ya Nishati Safi ya Kupikia nchini, Dk. Biteko amesema, watu wengi bado wanatumia nishati isiyo safi ya kupikia kama mkaa na kuni na wananchi wachache wanatumia gesi na umeme. Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa ndani ya miaka 10, asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia na serikali imepitisha Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia ikiwa ni moja ya njia za utekelezaji wa ajenda hiyo ambayo inanadiwa na Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.


Nipashe The Guardian

**Kutoka Menejimenti ya The Guardian Limited**



**Wapendwa Wateja wetu**

Tunayo furaha kutangaza hatua kubwa kuelekea upatikanaji wa magazeti yetu kidijitali. Kuanzia tarehe 13 Aprili 2024, magazeti ya wikiendi ya **Nipashe Jumamosi, Nipashe Jumapili na The Guardian on Saturday** yanapatikana kwa njia ya gazeti-mtandao kupitia **epaper.ippmedia.com** au **www.ippmedia.com**

Siku za wiki (Jumatatu hadi Ijumaa) utaendelea kufurahia matoleo yote, kuchapishwa na Mtandaoni

Asante kwa usomaji wako, na kuendelea kuwa nasi katika mabadiliko haya.

Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701
Subscription: 0625 174 714
Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz



Spika wa Bunge mstaafu na Mbunge wa jimbo la Kongwa, Job Ndugai (kushoto), akijadiliana jambo na Mbunge wa Monduli, Fred Lowasa Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Samia ajivunia ongezeko la biashara Tanzania, Uturuki

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema Tanzania na Uturuki, zimeshuhudia ongezeko la biashara kwa kipindi cha miaka 10 kutoka dola za Marekani milioni 60 mwaka 2011/2012 hadi dola za Marekani milioni 300 mwaka 2022/2023.

Alisema hayo jana nchini Uturuki wakati akihutubia wageni mbalimbali baada ya kutunukiwa Shahada ya Heshima ya Udaktari katika Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Ankara, nchini humo.

"Kama mwanachama wa G20, tunatarajia msaada wa Uturuki katika changamoto mbalimbali zinazoikabili Afrika yakiwamo madeni, mageuzi ya usanifu wa fedha duniani na kuhakikisha fedha za maendeleo endelevu ili kukabiliana na mapambano ya kuleta haki na usawa.

"Tumeendelea kuvutia washirika wanaoheshimika kufanya miradi ya kuleta mageuzi ya miundombinu nchini Tanzania, tunayo kampuni Yapi Merkezi kutoka katika nchi hii ya Uturuki, ambayo inashirikiana nasi katika kufanikisha mradi wetu wa treni ya kisasa (SGR)," alisema.

Rais Samia alisema hadi Desemba, mwaka jana, ilisajiliwa miradi mipya 526 mikubwa ya uwekezaji yenye thamani ya zaidi ya dola za Kimarekani bilioni 5.6, ambayo ni ongezeko la asilimia 58.

Kuhusu shahada aliyotunukiwa na kukabidhiwa na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ankara, Prof. Necdet Unuvat, kwenye hafla iliyofanyika chuoni hapo, Rais Samia alisema amepokea kwa niaba ya wachapakazi wote wa kike na wa kiume wa Tanzania.

"Ninapokea heshima hii kwa niaba ya wanaume na wanawake wachapakazi nchini Tanzania. Mimi ni kiongozi wao tu, na ninafanya yote ninayofanya kwa niaba yao. Ninapotafakari nyuma na kukumbuka changamoto na bidii ya watu wangu, ninajisikia unyenyekevu sana kukubali shahada hii ya heshima ya udaktari.

"Natoa shukrani zangu kwa Seneti ya Chuo Kikuu cha Ankara kwa uamuzi wao wa kunipatia Shahada ya Heshima ya Uzamivu katika Uchumi. Ninanyenyekea na kuheshimu kutambuliwa katika elimu hii ya kifahari ya chuo kikuu ambayo kimataifa inawekwa katika daraja la juu," alisema.

Rais Samia pamoja na viongozi wengine, waliwasili juzi nchini Uturuki kwa ziara ya kikazi.

# Ataka wabunge waonje joto la kikokotoo

**Na Vitus Audax,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalam, Kunti Majala, ameliomba bunge kujadili kupitisha kanuni mpya ya kikokotoo cha mafao kwa wastaafu ili ianze kutumika pia kwa wabunge kama wanaona kinafaa kuendelea kutumika kwa watumishi wanaostaafu.

Kunti alitoa rai hiyo bungeni jijini hapa jana wakati wa uchangiaji wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) mwaka 2024/25.

Alisema kuna haja ya serikali kuthamini mchango wa watumishi wanaolisadia taifa katika kada tofauti kabla na baada ya kustaafu.

"Kama kikokotoo tunakiona ni haki, hebu tuanze sasa tena mwezi wa sita kikokotoo kituhusu tuanze nalo humu ndani mwakani mwezi wa sita kituhusu."

"Si tunaona haki na ni sawa na hakina shida? Tuanze na sisi wabunge kutunziwa tupewe kidogo kidogo maana kwa sababu tunapokosa ubunge pia tunakuwa na maisha magumu zaidi hata ya hao watumishi tunaosema tuwatunzie fedha zao," alisema.

Mbunge huyo pia aliiomba serikali kuona umuhimu wa kutoa motisha kwa walimu na watumishi mbalimbali wanaokwenda kufanya kazi kwenye halmashauri zenye miundombinu isiyo rafiki kupewa motisha ya posho kutokana na kuishi katika mazingira magumu na wakati mwingine kuomba kuhama maeneo hayo.

"Suala lingine ni madai ya watumishi. Watumishi wana hali ngumu pamoja na mambo mengine walionayo kwanini hii stahiki yao wanayodai hatutaki kuwalipa, shida ni nini watu hawa wanadai haki yao wala siyo hisani na kama haiwezekani basi tuambie sameheni mmetoa msaada kanisani msikitini," alisema.

Naye Mbunge wa Tarime Vijijini (CCM), Mwita Waitara, alimtaka Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, kutokufumbia macho suala la kikokotoo bali aliwasilishe kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa watumishi wa Tanzania zaidi ya asilimia 60 wanahitaji kusikia mabadiliko.

"Watumishi wanahitaji kupata majibu namna tunavyopeleka unafuu katika kikokotoo, Wabunge tumeishasema lipokee kama hoja ya bunge kwa niaba ya watumishi na wastaafu kwani wanahitaji kuona linafanyiwa kazi na kabla ya bunge hili kuisha wapate majibu na kauli ya Rais," alisema Waitara.

# Kanuni kuwabana wazalishaji chupa za plastiki, vifungashio

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, amesema serikali imepanga kutunga kanuni mpya za utunzaji wa mazingira kwa wazalishaji wa vinywaji vinavyotumia chupa za plastiki na vifungashio.

Miongoni mwa kanuni ni pamoja na wazalishaji wa bidhaa hizo kukusanya chupa zilizotumika kutoka mitaani ili kutunza mazingira.

Jafo alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao cha majadiliano na wazalishaji wa bidhaa zinazofungashwa kwa plastiki kilichohusu kupata ufumbuzi wa tatizo la kuzagaa kwa chupa za plastiki mitaani.

Alisema madhara ya uharibifu wa mazingira kutokana na matumizi ya chupa za plastiki yanaathari nyingi kwa viumbe hai ikiwamo samaki baharini. Pia alisema bidhaa za plastiki zina madhara kwa mifugo na katika sekta ya utalii zinachafua mazingira ya hifadhi.

"Kila kampuni ihakikishe kuwa chupa zake hazipo mtaani baada ya matumizi. Na uamuzi huu utaongeza fursa ya ajira kwa vijana na wanawake watakaojiajiri kwa kuokota chupa hizo," alisema Jafo. "Marufuku hiyo inakwenda kutekelezwa kwa kuunda kanuni ya kuhakikisha ukusanyaji wa chupa za plastiki zilizotumika sio tena jambo la hiari," alisema Jafo.

Alimwagiza Katibu Mkuu Wizara ya Mazingira na taasisi zake kuhakikisha kanuni hizo zinakuwa tayari kabla ya kukamilika kwa vikao vya bunge la bajeti ambavyo vinaendelea jijini hapa.

Pia alilitaka Baraza la Taifa la Hofadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais kusimamia vyema kanuni za mazingira zilizopo.

Aliwataka wazalishaji hao kubuni vifungashio vinavyoweza kuharibiwa au kuzalishwa upya badala ya kuendelea na plastiki.

Alizipongeza kampuni zilizokamilisha taratibu za urejeshaji wa chupa za rangi na kuzitaka ambazo bado zianze kufanya hivyo.

Jafo alisema inaleta taswira mbaya kwa watalii wanaofika nchini na kutembelea fukwe mbalimbali kuona chupa za plastiki zikizagaa.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, anayeshughulikia Mazingira, Christina Mndeme, alisema ofisi yake inaendelea kuratibu na kusimamia masuala ya uhifadhi wa mazingira kuhakikisha kuwa yanatunzwa na kuwa salama kwa afya na ustawi wa kizazi cha sasa na kijacho. "Katika kuhakikisha kuwa uchafuzi wa mazingira unadhibitiwa, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali zikiwemo kuandaa sharia, kanuni na miongozo inayosimamia hifadhi ya mazingira," alisema.

Alisema ofisi hiyo inaendelea kusimamia katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki la Juni Mosi, 2019 na kuwa la mafanikio makubwa licha ya kuwapo changamoto ya taka za plastiki.

Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa NEMC, Dk. Thobias Richard, alisema licha ya katazo hilo kuna baadhi ya viwanda na wafanyabiashara wanafanya udanganyifu kwa kuzalisha bidhaa za plastiki zisizo na viwango.

"NEMC tulizunguka kwenye viwanda 89 vinavyozalisha chupa na mifuko ya plastiki, vipo 30 ambavyo tulikuta vina changamoto tukachukua hatia ikiwamo kuwapa elimu ili warudi kwenye utaratibu wa kisheria, tulienda kwenye fukwe, masoko 20 tukachukua hatua ka watu 89 walioshindwa kutekeleza agizo la serikali," alisema.

# Kesi matunzo ya watoto zaongezeka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATI ya mashauri 14,600 yaliyoshughulikiwa ya migogoro ya ndoa yaliyohusu masuala ya kifamilia na matunzo ya watoto yanaongoza kwa asilimia 41.

Mashauri hayo yalipokewa kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 na yaliyohusu masuala hayo ni 5,944 sawa na asilimia 41, migogoro ya ndoa yalikuwa 5,306 sawa na asilimia 36 na matunzo ya watoto waliozaliwa nje ya ndoa yalikuwa 3,350 sawa na asilimia 23.

Kutokana na hali hiyo, serikali imeelekeza mikoa na halmashauri kuandaa mijadala katika jamii kwa kutumia wataalamu wa malezi chanya ya watoto, familia, kuhusisha viongozi wa dini ili kutafuta ufumbuzi tatizo la malezi duni ya watoto na mmomonyoko wa maadili.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima akizungumza jana kuhusu maadhimisho ya siku ya kimataifa ya familia Mei 15, mwaka huu, alisema mashauri hayo yalifikishwa kupitia mabaraza ya kata na jumuiya na kwa mashauri 3,411 yalifikishwa kwa maofisa ustawi wa jamii 1,642 yalipatiwa ufumbuzi na 443 yanaendelea kufanyiwa kazi. Alisema mashauri 1,326 yalipewa rufaa kwenda kwenye vyombo mbalimbali vya usuluhishi ikiwamo mahakama (921) na mabaraza ya kata na jumuiya (405).

Kadhalika, alisema taarifa ya utafiti wa hali ya afya ya uzazi na mtoto na viashiria vya malaria nchini ya mwaka 2022, inaonesha asilimia 27 ya wanawake wa umri wa miaka 15 hadi 49 walifanyiwa vitendo vya ukatili wa kimwili.

"Asilimia 12 ya wanawake wa umri huo walifanyiwa ukatili wa kingono, asilimia 13 ya wanawake waliowahi kuwa na mume au mtu mwenye mahusiano katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti huo walifanyiwa vitendo vya ukatili wa kimwili, kingono na kihisia," alisema.

"Unyanyasaji wa kimwili, kingono, au kihisia miongoni mwa wanawake walioolewa umepungua kutoka asilimia 50 mwaka 2015/16 hadi asilimia 39, mwaka 2022/23."

Alitaja moja ya vikwazo katika kukabiliana na migogoro ya familia ni kukosekana kwa upendo, ustahimilivu na kutokuwa na hofu ya Mungu miongoni mwa wanafamilia.

Aidha, alisema mifumo kandamizi inayoendelea katika jamii inayochochewa na mila na desturi za baadhi ya makabila nchini zimesababisha wanandoa hasa wanawake kukaa kimya bila kujadiliana na kumaliza tofauti zao jambo linaloweza kuwa na athari kubwa.

"Mara zote waathirika wakubwa huwa ni watoto. Vikwazo vingine ni uelewa mdogo kuhusu malezi chanya na mawasiliano duni miongoni mwa wanafamilia pamoja na wazazi kutotimiza majukumu yao ya msingi ya malezi. Changamoto hizi zimechochea mmomonyoko wa maadili," alisema.

Alisisitiza wizara imeendelea kuratibu huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia kupitia Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii lililopo Makao Makuu ya Wizara.

Dk. Gwajima alisema, katika kuadhimisha siku hiyo aliwaomba viongozi wa dini watumie nyumba za ibada kutoa ujumbe kuhusu umuhimu wa malezi bora ya watoto kujenga familia imara na taifa imara.

# Serikali yaweka ngumu uraia pacha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema bado haiko tayari kuwa na utaratibu wa kutoa uraia pacha badala yake iko katika hatua za mwisho kukamilisha utoaji wa hadhi maalum kwa raia wa nchi nyingine wenye asili ya Tanzania, ili kuwezesha kuchangia maendeleo ya taifa.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Afrika Mashari, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, alisema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafaniko ya wizara hiyo katika kipindi cha miaka 60 ya Muungano.

"Mchakato huo unatarajiwa kukamilika baada ya Bunge la Jamhuri ya Muungano kukamilisha kufanya marekebisho ya Sheria za Ardhi na Uhamiaji ndipo hadhi maalum itaanza kutumika rasmi," alisema Balozi Mbarouk.

Aidha, alisema wizara imekamilisha mfumo wa kidijitali wa kukusanya na kutunza taarifa za diaspora unaofahamika 'Diaspora Digital Hub'.

"Mpaka sasa diaspora wa Tanzania wapatao 1,403 wamejiandikisha katika mfumo huo na hivyo kuiwezesha serikali kupata takwimu sahihi za idadi, mahali walipo, ujuzi na uzoefu walionao.

"Mfumo pia utawezesha diaspora kupata taarifa kuhusu fursa na huduma mbalimbali zinazotolewa na serikali na sekta binafsi nchini, lakini pia mfumo huu unawasaidia kuwapunguzia usumbufu wa kwenda kwenye balozi au kutuma barua kwa ajili ya kujiandikisha," alisema.

Kadhalika, alisema katika kipindi hiki cha miaka 60 ya Muungano serikali imefanikiwa kuimarisha ushiriki wa Watanzania waishio nje ya nchi raia wa nchi nyingine wenye asili ya Tanzania katika maendeleo ya taifa.

Alisema miongoni mwa mafanikio hayo ni serikali kuchukua hatua za kisera kwa kujumuisha masuala ya diaspora katika mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001.

"Katika kipindi hiki, Tanzania inajivunia mchango wake katika juhudi za kulinda amani duniani kama hatua ya utekelezaji wa malengo ya Sera Mpya ya Mambo ya Nje na mojawapo ya malengo mahsusi ya Umoja wa Mataifa (UN)," alisema.

Alisema Tanzania imekuwa ikishiriki katika kulinda amani kupitia Misheni za Kikanda ikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa.

Alisema baadhi ya maeneo ambayo Tanzania imechangia walinda amani ni pamoja na Lebanon, Darfur, Abyei, Liberia, Sudan Kusini, Sudan, DRC, Msumbiji na Afrika ya Kati.

"Kwa upande mwingine, Tanzania imeshiriki kikamilifu utatuzi wa migogoro kwa njia ya mazungumzo na diplomasia kwenye nchi na maeneo mbalimbali ikiwamo, Darfur, Cambodia, Sudan Kusini, Burundi na Kenya," alisema.


**OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI**

**MJI WA SERIKALI-MTUMBA 1 BARABARA YA ARDHI, S.L.P. 104, 40403 DODOMA.**

**info@planninginvestment.go.tz**

**SHINDANO LA KUBUNI NEMBO, JINA NA KAULIMBIU YA TAASISI.**

*"Shiriki Mapinduzi ya Uwekezaji Tanzania"*

Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania imeamua kuunganisha Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Eneo Maalumu la Uwekezaji na Mauzo Nje ya nchi (EPZA). Kuunganisha huko kunapelekea kuzaliwa kwa taasisi mpya, itakayobeba jukumu la kurahisisha na kukuza uwekezaji, kuongoza kwa ustadi na kusimamia maendeleo ya maeneo maalum ya kiuchumi na uzalishaji kwa ajili ya kuuza nje.

Kufuatia hatua hii; Mwaliko unatolewa kwa wabunifu binafsi na taasisi kubuni na kusanifu **Jina, Nembo na Kaulimbiu** ya taasisi (Mamlaka) hii mpya nchini.

**Jina, Nembo na Kaulimbiu** pendekezwa ziwe na sifa zifuatazo;

- Kujumuisha na kuakisi shughuli na majukumu ya TIC na EPZA.
- Kuwa na mwonekano na mvuto wa kipekee.
- Kutamkwa na Kueleweka kirahisi.
- Kuwa na uwezo wa matumizi anuwai na mtambuka.
- Kutokuwa na mfanano au uhusiano na Jina, Nembo na Kaulimbiu ya taasisi nyingine.
- Kuzingatia utamaduni na maadili ya kitanzania.

Shindano hili ni kwa Mtanzania yeyote mwenye umri wa miaka 18 au zaidi .

**Zawadi:**

- Mshindi wa Kwanza: **Tsh. 3,000,000/-**
- Mshindi wa Pili: **Tsh. 2,000,000/-**
- Mshindi wa Tatu: **Tsh.1,000,000/-**

**MUHIMU:** Tafadhali wasilisha **ubunifu wako kwa mfumo wa pdf,** ukiambatanisha jina lako kamili na namba ya simu kwa: **tic.epza@tic.go.tz** kabla ya **tarehe 22 Aprili 2024 saa 09: 30 Alasiri.**

Kwa maelezo zaidi kuhusu TIC na EPZA, tembelea tovuti zifuatazo:
**www.tic.go.tz au www.epza.go.tz.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ulaji unaofaa utapunguza magonjwa yasiyoambukiza

**MAGONJWA** yasiyoambukiza limekuwa tatizo kubwa kwa watanzania wengi kwasababu ya kutozingatia kanuni za afya ikiwamo ulaji unaofaa.

Kutokana na shughuli mbalimbali wanazojishughulisha, Watanzania wengi wanajikuta wanakula vyakula vya ovyo vinavyopikwa mitaani na hata vinavyopikwa majumbani havizingatii kanuni.

Idadi ya watu wanaoongezeka miili kwa kutozingatia ulaji unaofaa inasababisha kuibuka kwa magonjwa hayo yasiyoambukiza yakiwamo ya shinikizo la damu, moyo, kisukari na mengine.

Imeelezwa kuwa Mtanzania mmoja katika watatu ana uzito uliokithiri na watu wenye elimu na uhakika wa kipato wako kwenye kundi la waathirika zaidi.

Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Magonjwa yasiyoambukiza (NDC), katika Wizara ya Afya, Dk. Omary Ubuguyu, anaeleza katika maeneo machache ambayo Watanzania wanafanya vizuri ni kwenye mazoezi kwa sababu kumekuwa na mwamko mkubwa wa watu kukimbia, kutembea na mbio za marathoni nyingi.

Hata hivyo, inaelezwa katika masuala ya ulaji bado ni watu saba katika 100 ambao wanazingatia ulaji unaofaa.

Ukipita barabarani unaweza kukutana na mwanamke ukadhani ni mjamzito, lakini kumbe ana kiribatumbo kinachosababishwa na ulaji usiofaa au unywaji pombe uliopitiliza.

Inaelezwa kuwa suala la uzito na unene kupita kiasi hali imezidi kuwa mbaya, zamani ilikuwa ni katika kila watu wanne, mmoja ana uzito uliokithiri, sasa hivi ni mtu mmoja katika kila watu watatu ana uzito au unene uliokithiri.

Watalaamu wa afya wanaeleza kuwa vijana wanaathirika zaidi kuliko rika nyingine yoyote na wanawake wanaathirika zaidi kuliko wanaume katika ulaji usiofaa na unywaji pombe. Yaani watu wenye umri mdogo na wanawake ndio wako kwenye uhatarishi zaidi na inamaanisha kwamba jamii ipo katika hali ngumu sana.

Utafiti unaonesha magonjwa yasiyoambukiza kama saratani, kisukari, figo na shinikizo la juu la damu, yanaathiri zaidi watu wenye kipato cha chini, lakini ni kinyume chake katika baadhi ya nchi kama Tanzania ambako waathirika wakubwa ni wasomi na wenye uhakika wa kipato.

Wafanyakazi ndio wanaotumia vyakula vya viwandani zaidi, pombe zaidi, ndio watu wenye fursa ya kununua soda na vitu vingine ambavyo vinaathiri afya.

Aidha, wafanyakazi wanaathirika zaidi kutokana na mtindo wa maisha kwa kuwa hawana nafasi ya kupata chakula bora kutokana na kununua vyakula wasivyojua namna vilivyoandaliwa na pia hawapati nafasi ya kufanya mazoezi.


Hali hii inasababisha taifa kuwa na mzigo mkubwa wa magonjwa yasiyoambukiza. Gharama katika matibabu kwa mfano Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), vitu vikubwa vinavyoelemea taifa ni kutibu magonjwa kama saratani, matatizo ya figo, shinikizo la juu la damu, kiharusi na kisukari.

Njia ya kuondokana na tatizo hilo ni watu kujitahidi kufanya mazoezi kila siku, kula vyakula vyenye virutubisho, kupima afya mara kwa mara na kubadili mtindo wa maisha unaochochea magonjwa yasiyoambukiza.

Pia, waajiri wanapaswa kuhakikisha usalama mahala pa kazi na afya kuwa kipaumbele namba moja ili wafanyakazi waweze kufanya uzalishaji unaokusudiwa.

Mlo kamili unaopaswa kuzingatiwa kila siku na aina yake kwenye mabano ni wanga (ugali, wali au ndizi), mboga (kabichi, spinachi, mchicha au figiri), protini (nyama, samaki, kunde, njegere na maharage), matunda (embe, chungwa, papai au tikiti), vitamini (karanga au korosho) na maji ya kutosha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tahadhari ya pundamilia itutawale sote madereva, hadi tunaotembea

Na Christina Mwakangale

**PUNDAMILIA** au zebra ni eneo linalotumika kwa ajili ya watembea kwa miguu kuvuka kwenye barabara.

Katika barabara yeyote ni lazima kuwepo na alama hizi ambazo zinawaongoza watembea kwa miguu kufahamu pa kuvukia na si kuvuka kiholela.

Pia wenye vyombo vya moto yaani magari, pikipiki, baiskeli zinatakiwa kuyafahamu maeneo haya na kuzingatia au kuwa makini zaidi wafikapo maeneo haya.

Kwenye miji na majiji makubwa nchini kuna ongezeko kubwa la magari, huku baadhi ya madereva baadhi yao wakionekana kupuuza alama za barabarani hususan pundamilia.

Wanadhani alama hiyo haiwahusu kwa kuwa kwa wakati huo wao wanatembelea kwa miguu minne yaani kwa kutumia gari, kuwasahau wanaotembea kwa miguu.

Baadhi yao madereva wanaziheshimu alama hizo, wakizingatia yale mafunzo waliyoyapata vyuoni kwamba alama za barabarani zina umuhimu kulingana na mazingira.

Kupuuza alama za barabarani kuna madhara kwani kunaweza kusababisha ajali ambazo zingeepukika, iwapo dereva atakuwa makini.

Wapo baadhi yao ambao wakiwa barabarani, kwao mtembea kwa miguu atajijua mweyewe, kiasi kwamba hata palipo na haki ya kuvuka kutoka upande mmoja kwenda mwingine, hupuuzwa.

Embu fikiria kuna watoto wadogo wangapi ambao kila siku wanazitumia barabara hizi, alafu wakutane na dereva ambaye hathubutu kuheshimu pundamilia.!

Wanafunzi pia ni kundi mojawapo kubwa zaidi ambalo linatumia barabara hizi, kwa kwenda shule na kurudi nyumbani kila siku, achilia mbali wafanyakazi.

**Baadhi yao madereva wanaziheshimu alama hizo, wakizingatia yale mafunzo waliyoyapata vyuoni kwamba alama za barabarani zina umuhimu kulingana na mazingira.**

Kuna kundi la watu wanaoishi na ulemavu, wazee ambao wanahitaji kuvuka pia katika barabara hizi na kwenda kufanya shughuli zao za kujitafutia kipato kila siku.

Kwa nchi zilizoendelea maeneo haya huheshimiwa na kamera hufungwa maeneo haya ili kuwakamata watu kama hawa ambao hudhani kuwa mwenye haki ya kutumia barabara ni yeye peke yake.

Baadhi ya madereva pale anapoiona alama ya pundamilia mita chache kutoka pale alipo anaongeza mwendo au kama yupo katika foleni anasimamisha gari juu ya pundamilia bila hata ya wasiwasi.

Pundamilia zina umuhimu mkubwa kwa watembea kwa miguu, wanahitaji kuheshimiwa na dereva aheshimu alama hizo.

Ustaarabu wa mtu huanzia na mtu mwenyewe kuwa unapokuwa dereva jaribu kuheshimu alama za pundamilia kwa kuwapisha watembea kwa miguu kuvuka kwani wao pia wanawahi katika majukumu yao ya kila siku na shughuli nyingine za ujenzi wa taifa.

Alama hizi zinawekwa na wataalamu wanaojenga hizi barabara kwa kufahamu kwamba, barabara hutumiwa na wengi wakiwamo watembea kwa miguu.

Ajali zinaweza kupungua na kunusuru maisha ya watu iwapo hatua kama hizi zitachukuliwa kwa madereva kuwa makini katika maeneo haya, kwa kuzingatia alama za barabarani.

Kupuuza alama za barabarani kwako dereva, kumbuka unaondoa haki ya watumiaji wengine wa barabara.

HABARI KITAIFA

## CAG abaini kiini wafungwa kurudia makosa

**Na Romana Mallya**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini kiini cha wafungwa wengi kurudia makosa wanapotoka gerezani.

Anakitaja kiini hicho katika ripoti yake ya ukaguzi wa ufanisi kwa mwaka 2022/23, iliyowasilishwa bungeni Jumatatu.

Ni ripoti inayotolewa kipindi ambacho kumekuwa na matukio ya wafungwa, wakiwamo wanaoachiwa kwa msamaha wa Rais, kurudia kufanya makosa wanaporejea uraiani, hata kuibua maswali "wanafundishwa nini gerezani?"

Katika ukaguzi wake, CAG Charles Kichere, amesema serikali imefanya jitihada mbalimbali za kuboresha programu za urekebishaji wafungwa kwa kuanzisha Kitengo cha Huduma za Urekebu wa Wafungwa chini ya Jeshi la Magereza Tanzania.

Vilevile, Jeshi la Magereza lilianzisha gereza la shule ya ufundi, Ruanda - Mbeya na gereza la vijana, Wami - Morogoro, na kuanzisha Stashahada ya Sayansi ya Urekebu kwa Maofisa Magereza katika Chuo cha Mafunzo ya Urekebu Tanzania.

CAG anataja maeneo yanayohitaji maboresho zaidi kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa kiwango cha wafungwa wanaorudia makosa kwa wastani wa asilimia 1.5 kuanzia mwaka 2019 hadi 2023.

Anasema ukaguzi ulibaini ongezeko la wafungwa wanaorudia makosa kwa wastani wa asilimia 1.5 kuanzia mwaka 2019 hadi 2023, licha ya mipango ya urekebu.

"Hali hii inaonesha kuwa wafungwa zaidi wanarudi kwenye kufanya uhalifu. Kiwango cha kurudia kufanya makosa kilikuwa hakiendani na muda wa wafungwa gerezani. Wafungwa wengi zaidi walio na hukumu fupi walirudia makosa," CAG anaeleza.

Kati ya mwaka 2019 na 2023, hali ya wafungwa waliorudia kufanya makosa ni asilimia 59.22, walikuwa wafungwa waliohukumiwa kifungo cha chini ya mwaka mmoja; asilimia 24.65 walikuwa waliohukumiwa kifungo cha kuanzia mwaka mmoja hadi miaka mitatu.

"Asilimia 10.14 walikuwa wafungwa waliohukumiwa kifungo cha kuanzia miaka mitatu hadi mitano; na asilimia 3.09 walikuwa wafungwa waliohukumiwa kifungo cha kuanzia miaka mitano hadi 10," alisema.

Aidha, asilimia 0.37 walikuwa wafungwa waliohukumiwa kifungo cha kuanzia miaka 10 hadi 15; asilimia 2.22 walikuwa wafungwa waliohukumiwa kifungo cha kuanzia miaka 15 hadi 20; asilimia 0.32 walikuwa wafungwa waliohukumiwa kifungo cha kuanzia miaka 20 hadi 30; na asilimia 0.01 walikuwa wafungwa waliohukumiwa kifungo cha zaidi ya miaka 30.

**KIINI CHA TATIZO**

CAG anasema hali hiyo ilisababishwa na ukosefu wa mitaala na miongozo ya magereza kwa ajili ya uendelezaji rasmi wa mipango ya urekebu; uainishaji na utengano wa wafungwa kujikita kwenye jinsia na umri pekee; miundombinu isiyotosheleza ya uainishaji; shughuli za msingi za gereza kuamua uainishaji; na ukosefu wa sera na miongozo ya uainishaji wa wafungwa.

Pia, anataja kukosekana kwa mipango rasmi ya kuunganisha wafungwa wanaotarajia kukamilisha vifungo vyao.

CAG anafafanua kuwa ukaguzi wake ulibaini kuwa licha ya kuwapo programu za urekebu, hakukuwa na mpango rasmi wa kuwaandaa wafungwa wanaokaribia kukamilisha muda wao wa kifungo ili kuwaandaa kukabiliana na jamii watakayoenda kuishi ikiwemo changamoto kadhaa zinazoweza kuwapata katika kipindi hicho.

"Kukosekana kwa mfumo huu maalum wa kuwaandaa wafungwa, kunasababisha wafungwa kuachiwa bila kuandaliwa, hivyo kuwapa ugumu wa kupata huduma za jamii na misaada mbalimbali na kuchangia ongezeko la wafungwa wanaorudia makosa," CAG anawasilisha hoja yake.

Katika ripoti hiyo, CAG anabainisha kuwa kwa mwaka 2023 pekee wafungwa 3,262, walirudia makosa baada ya kutoka gerezani, wengi wao wakiwa ni walioachiwa huru baada ya kutumikia vifungo vifupi.

Pia, anaeleza, ukaguzi wake ulibaini uainishaji wa wafungwa katika magereza saba aliyotembelea unajikita zaidi kwenye jinsia na umri pekee, masuala mengine kama asili ya kosa, historia ya uhalifu na umuhimu wa urekebishaji hayazingatiwi.

"Ukaguzi pia ulibaini wafungwa na maabusu waliwapo katika magereza ambayo yalipangwa na kujengwa kwa ajili ya maabusu pekee.

"Hali hii ilisababishwa na miundombinu usiyotosheleza ya kusaidia uainishaji wa wafungwa na kutokuwapo sera na miongozo ya uainishaji wafungwa," CAG anasema.



Mchuuzi wa mboga za majani akiziandaa wakati akisubiri wateja katika soko la Kinyerezi, jijini Dar es Salaam jana. Fungu la mboga linauzwa kwa bei ya 500/- hadi 1,000/-. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Prof. Kitila Mkumbo ataja mambo ya kujivunia miaka 60 ya Muungano

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo ametaja mambo ya kujivunia katika miaka 60 ya Muungano, ikiwamo kuongezeka wastani wa umri wa kuishi kwa Watanzania kutoka miaka 32 hadi 66 huku wanawake wakionekana kuishi miaka mingi kuliko wanaume.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu mafanikio ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Prof. Mkumbo alisema, ustawi wa wananchi na nchi umeimarika ndani ya miaka 60 ya Muungano na wastani wa umri wa kuishi kwa Watanzania umeongezeka kutoka wastani wa miaka 32 wakati wa Muungano hadi kufikia miaka 66 mwaka 2022 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyikamMwaka 2022 na ifikapo mwaka 2025 inatarajiwa kufikia miaka 68.

Alifafanua kuwa katika sensa hiyo imeonesha wanawake wanaishi miaka mingi na umri wao wa kuishi umefikia wastani wa miaka 68 kuliko wanaume ambao ni miaka 64.

Alisema kuwa kuongezeka kwa umri huo kumetokana na nchi kupiga hatua kuhakikisha Muungano unakua hai na unadumu, ikiwamo kulinda na kudumisha amani, utulivu na mshimano ambao ni msingi wa maendeleo huku usalama wa chakula ukiongezeka kutoka asilimia 60 ambao kwa sasa ni asilimia 124 wakati lengo likiwa ni kufikia asilimi 130 ifikapo mwaka 2025.

Kadhalika, kuimarika ustawi wa wananchi na nchi kumetokana na serikali kuwekeza kwenye sekta ya elimu kwa kuhakikisha elimu msingi kuwa ya wote na uandikishaji wa wanafunzi wa shule ya msingi umefikia asilimia 105, sekondari ni asilimia 70 wakati lengo lilikuwa asilimia 48 ifikapo mwaka 2025.

"Serikali imewekeza kwenye sekta ya afya ambapo huduma za afya ya mama kuimarika na kupunguza vifo vya mama kutoka vifo zaidi ya 1,000 hadi vifo 104 kwa sasa kati ya vizazi hai 100,000 huku vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua kutoka vifo 95 kati ya vizazi hai 1000 mwaka 2000 hadi kufikia vifo 43 kwa sasa, huduma ya upatikanaji maji vijijini imeongezeka kutoka chini ya asilimia 50 kabla ya Muungano hadi kufikia asilimia 72 kwa sasa," alisema.

Akizungumzia uchumi, Prof. Kitila alisema, kwa miaka 20 iliyopita wastani wa ukuaji wa uchumi ulikuwa mzuri kati ya asilimia sita hadi saba na hiyo inatokana na kuimarika kwa miundombinu ya barabara na mtandao wa Barabara za lami na zege kuongezeka kutoka kilomita 4,179 hadi 11,969 kwa mwaka 2022.

Pia, upatikanaji wa huduma za nishati ya umeme umeongezeka kutoka kuwa kata 10 kati ya 100 zilizokuwa na umeme hadi kufikia kaya 80 kati ya 100 kuwa na nishati hiyo kwa sasa wakati lengo lilikuwa ni kaya 90 ifikapo mwaka 2025.

"Tumefanikiwa katika Muungano kwasababu tupo, pia tumefanikiwa kulinda amani, utulivu na mshikamano, tumepiga hatua kwenye ustawi wa jamii na uchumi tunakwenda vizuri kwasababu ni msingi wa maendeleo na visababishi vya uchumi vinakwenda vizuri."

"Tuna mengi ya kujivunia katika Muungano wetu kuliko ya kusikitishwa, tumepitia changamoto na zinaweza kutokea nyingi, lakini kutokana na uongozi wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, chini ya Rais Samia uko vizuri kujizatiti kupambana na changamoto zitakazoweza kujitokeza ambazo zinaweza kutishia Muungano wetu, tunaamini utadumu kwa miaka 60 mingine ijayo," alisema.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Miongozo taarifa binafsi hadharani

**Na Zanura Moleli**

TUME ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), imetoa miongozo minne katika utekelezaji wa majukumu yake.

Miongozo hiyo ni wa usajili wa wakusanyaji na wachakataji wa taarifa, kusimamia malalamiko, sera ya ulinzi wa taarifa binafsi, na idhini ya mhusika wa taarifa.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasilino PDPC, Innecent Mungy, muundo huo umekamilika na kuidhinishwa na kwamba majukumu yatatekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar katika masuala yanayohusu Muungano.

Alisema mfumo wa kusajili wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi una uwezo wa kufanya mambo mbalimbali, ikiwamo utambuzi na usajili wa wakusanyaji taarifa (data controller), wachakataji taarifa (data processor) na kutoa vyeti vya usajili (registration module).

Mungy alisema kanuni mbili zimetungwa chini ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Na. 11 ya mwaka 2022 na zilikwisha kutangazwa katika Gazeti la Serikali (GN 3049) Mei12,2023 ikiainisha utaratibu wa mhusika wa taarifa kupata haki katika ukusanyaji na uchakataji wa taarifa zinazomhusu.

"Utaratibu wa usafirishaji wa taarifa binafsi nje ya nchi unawataka wahusika binafsi wa taarifa kuhakikisha uwekaji wa viwango vya usalama wakati wa ukusanyaji na uchakataji.

"Kanuni ya taratibu za kushughulikia malalamiko ya ukiukwaji wa misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi GN 350 Mei 12,2023 inafafanua utaratibu wa kuwasilisha malalamiko dhidi ya ukiukwaji huo,kwa kuzingatia uchunguzi na usuluhishi wa lalamiko lililowasilishwa pamoja na taratibu za kusikiliza malalamiko,"alisema.

Aidha, alisema tume hiyo imeunda bodi yenye wajumbe saba na majukumu yake yamezingatia misingi ambayo nchi zote duniani zinatekeleza katika kuhakikisha taarifa binafsi za watu zinalindwa.

Majukumu ya tume hiyo, alisema ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa sheria, kusajili wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi, kupokea, kuchunguza na kushughulikia malalamiko kuhusu madai ya ukiukwaji wa ulinzi wa taarifa binafsi na faragha za watu, kufanya tafiti na kufuatailia maendeleo ya teknolojia kuhusiana na uchakataji wa taarifa pamoja na kuimarisha mashirikiano na nchi zingine.

Pia alisema kukua kwa teknolojia ya mawasiliano duniani kunatajwa kuchangiwa usafirishaji wa taarifa binafsi kutoka nchi moja kwenda nyingine bila kuzingatia taratibu za ulinzi wa taarifa binafsi iliyokubalika duniani.

"Tanzania ni mwachama wa jumuiya mbalimbali za kikanda na kimataifa zikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Afrika (AU). Nchi wanachama zimekubaliana kuwa na sheria mahususi na taasisi huru katika kukabiliana na changamoto hiyo," alisema.

Mungy alisema EAC iliandaa mwongozo wa usalama mtandaoni mwaka 2008, SADC iliandaa sheria tatu za mfano za usalama mtandaoni mwaka 2012 na AU iliandaa mkataba wa Umoja wa Afrika kuhusu usalama mtandaoni na ulinzi wa taarifa binafsi (Malabo) mwaka 2014. Mikataba hiyo kwa ujumla inawataka nchi wanachama kuwa na sheria tatu za msingi za usalama wa mtandao na taasisi huru.

Takwimu zinaonyesha kati ya nchi 198 duniani, 162 zimetunga sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi, nchi 36 kati ya 54 za Afrika tayari zimetunga sheria hiyo, 12 kati ya 16 za SADC zimeshatunga na nchi nne kati ya sita za EAC zimetunga sheria hiyo huku Burundi na Sudan Kusini zikiwa kwenye mchakato wa utungaji wa sheria.

Alisema Tanzania imekamilisha utungaji wa sheria hizo za msingi ambazo ni Sheria ya Makosa Mtandaoni ya Mwaka 2015, Sheria ya Miamala ya Kielektoniki ya Mwaka 2015 na Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022. Tume hiyo ilizinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Aprili 3, mwaka huu.

"Tume hii ni chombo muhimu katika maendeleo ya nchi kiuchumi hususani katika kipindi hiki ambacho dira ya nchi ni uchumi wa kidijitali ambapo taarifa imekuwa bidhaa muhimu," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Dustan Kyobya (wa pili kulia), akizungumza kabla ya kupokea msaada wa vyakula vyenye thamani ya Sh. milioni 14 kutoka kampuni ya Sukari Kilombero, wilayani humo, mkoani Morogoro, jana kwa ajili ya waathirika wa mafuriko. Kulia ni Meneja Mawasiliano wa kampuni hiyo, Victor Gemelwa. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

# Sukari Kilombero washika mkono waathirika mafuriko

**Na Christina Haule,** KILOMBERO

KAMPUNI ya Sukari Kilombero, mkoani Morogoro imetoa msaada wa tani sita za vyakula zenye thamani ya Sh. milioni 14 kwa waathirika wa mafuriko wilayani Kilombero.

Meneja wa Mawasiliano na Mahusiano kutoka kampuni hiyo, Victor Gemelwa, alitoa msaada huo mbele ya Kamati ya Ulinzi na Usalama wilayani humo wakati wakiwashika mkono waathirika wa mafuriko katika kutimiza wajibu wao wa kurejesha faida kwa jamii.

Vyakula hivyo kuwa ni tani mbili za unga wa mahindi, tani mbili za maharage na mbili za mchele ambazo wamezifunga kwenye kilo tano kwa kila mfuko zitakazogawiwa kwa kila kaya iliyoguswa kwa wananchi 500 waliopata athari za mafuriko. Aidha, Gemelwa aliishukuru serikali inavyochukua hatua za haraka ikiwamo kurejesha miundombinu katika hali yake ya kawaida huku wakiwahamashisha wadau kuonesha ushirikiano wa kutoa msaada kwa waathirika hao.

"Na sisi kwetu sera yetu inahusisha maisha au jamii tunayohudumia na leo pia tupo katika kutekeleza wajibu wetu wa moja kwa moja na tutoe wito kwa wadau wengine kuona haja ya kujitoa kusaidia waathirika hawa, na tunafahamu haya yanatokana na athari za mabadiliko ya tabianchi," alisema Gemelwa. Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Dastun Kyobya, alikishukuru kiwanda hicho kwa kutoa msaada huo uliokuwa kwenye mfumo kamili wa ugawaji ambao utagawiwa kwa wakazi wa maeneo ya Utengule na Masagati ambako mawasiliano yamekatika na kupelekewa chakula kwa kutumia helikopta.

Aidha, alimshuruku Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa nao bega kwa bega tangu wamepata majanga hayo ya mafuriko ikiwamo ajali ya treni kwa watu 544.

Alisema pia alituma helkopta kwa ajili ya kupeleka chakula kwenye maeneo la Masagati na Utengule huku akituma kamati ya maafa ikiambatana na mawaziri zaidi ya 10 na makatibu wakuu na kujionea hali ya mazingira.

# Zaidi watoto mil. 1 kufikiwa mradi lishe

**Na Adela Madyane,** KIGOMA

WATOTO milioni 1.2 wenye umri wa chini ya miaka mitano watafikiwa na mradi wa lishe kukabiliana na tatizo la udumavu katika mikoa ya Njombe, Songwe, Rukwa, Katavi na Kigoma.

Mkurugenzi wa mradi wa lishe, Joyceline Kaganda, alisema hayo katika hafla ya uzinduzi wa mradi huo uliofanyika mkoani hapa unaotekelezwa kwa miaka mitano kuanzia Oktoba 2023 hadi Septemba 2028.

Alisema mradi huo unaofadhiliwa na Shirika la kimataifa la Maendeleo la Marekani (USAID), unagharimu Dola za Kimarekani milioni 39,000 ambao unatarajiwa kuleta mabadiliko katika afya za watoto na wanawake ambao mpaka sasa wanakabiliwa na utapiamlo kwa asilimia 30.

Mradi unalenga kuangalia mambo mbalimbali ikiwamo ubora wa huduma za lishe kwenye vituo vya afya, upatikanaji wa majisafi na salama, ulaji wa chakula chenye virutubisho na kuongeza uwezo wa halmashauri katika matumizi ya takwimu.

"Mradi unatarajia pia kutoa elimu juu ya mabadiliko ya tabia ya namna ya uandaaji wa chakula cha mtoto, elimu ambayo itakuwa inatolewa katika siku ya afya ya kijiji ambapo wanawake wataelekezwa namna ya kuandaa chakula hicho kwaajili ya kupata afya bora," alisema Kaganda.

Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Lishe kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Patric Codjia, akiwakilisha wadau wa lishe nchini, alisema takwimu za sensa za mwaka 2022, zinaonesha jitihada za serikali za kupunguza udumavu licha ya kuwapo kwa changamoto ya matumizi mabaya ya chakula ikiwa ni moja ya sababu kuu ya udumavu katika mikoa hiyo.

"Wanawake wengi wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa chakula bora, wengine wanapata chakula cha msimu, wengine hawana ufahamu wa lishe bora ya utotoni na wengine wanapata changamoto namna ya kufika katika kliniki zenye huduma ya lishe, yote haya yanasababisha udumavu, tunaamini kupitia mradi wa USAID Lishe tutafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na serikali za mitaa na sekta binafsi kutatua changamoto hizo," alisema Codjia.

Eliuta Kivele, mwakilishi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, alisema mradi huo ni muhimu kwakuwa unaandaa watu watakaokuwa tayari kushiriki katika maendeleo ya nchi na utachangia utekelezaji wa mpango jumuishi wa utekelezaji wa afya na lishe kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2021/2026.

Craig Hart, Mkurugenzi wa misheni kutoka USAID amefurahishwa na matokea ya ufadhili wanaoutoa kwa nchi ya Tanzania kwa kutoa matokea chanya katika afya akitoa mfano wa namna umri wa kuishi wa Watanzania ulivyoongezeka kwa miaka 15 kuanzia mwaka 2000-2019 kupitia miradi ya afya yenye lengo la kuokoa maisha.

"Kwa kipindi cha miaka 20 iliyopita, USAID imetoa dola bilioni 7.5 katika sekta ya afya nchini, tunajivunia kuona Serikali ya Marekani inaendelea kuwa kinara katika kuhudumia jamii kwa kubadili afya za Watanzania na zaidi kulingana na matokeo chanya ya kuokoa maisha ya watu," amesema Hart.

Akizungumzia upande wa lishe, Hart amesema kwa kipindi cha miaka 10, wamewekeza jumla ya dola milioni 600 katika sekta ya lishe na kuwataka viongozi wa mikoa wanaotekeleza mradi wa lishe kujifunza namna Morogoro, Iringa na Manyara walivyoweza kupunguza changamoto ya udumavu kati ya asilimia 35-49 ili nao wapate matokea tarajiwa kwaajili ya mradi.



# Shahidi kesi ya uporaji: Washtakiwa walikuwa na kesi nyingine ya mauaji

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SHAHIDI muhimu wa Jamhuri katika kesi ya unyang'anyi wa kutumia silaha inayomkabili Eben Mwaipopo (27) na Fredrick Mkwembe au 'Samora white,'ameieleza Mahakama ya Wilaya ya Moshi, kwamba washtakiwa hao licha ya kupora bastola ya mfanyabiashara maarufu wa Moshi, Denis Swai, walikuwa wakikabiliwa na kesi nyingine ya mauaji mkoani Tanga.

Shahidi huyo wa upande wa mashtaka, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Benedicto Petro kutoka Tanga, alikuwa akitoa ushahidi jana katika Mahakama ya Wilaya ya Moshi, akiongozwa na Wakili Mwandamizi wa Serikali, Kambarage Samson anayesaidiwa na Imelda Mushi na Amina Mkayala.

Akiwa mbele ya Hakimu Mkuu Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Ruth Mkisi anayesikiliza kesi hiyo Namba 231 ya Mwaka 2022, alidai kuwa washtakiwa hao walichukuliwa na maofisa wa polisi Kilimanjaro kutoka Tanga, Juni 6 mwaka 2022, ambako walikuwa wakikabiliwa na kesi ya mauaji ya mlinzi wa shamba la mkonge.

Mfanyabiashara Denis Swai, aliibiwa silaha hiyo Juni 28 mwaka 2017 katika eneo la Soweto, Wilaya ya Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro.

Katika kosa la kwanza la unyang'anyi wa kutumia silaha, ambalo ni kinyume na Kifungu cha 287 (A) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Mwaka 2019, washtakiwa hao wanadaiwa kuiba bastola aina ya Norinco, yenye thamani ya Sh.350, 000 ikiwa na risasi 27 zenye thamani ya Sh.75, 600 na Paundi 30,000, sawa na Sh. milioni 79, 650,000 na mashine ya kupima damu yenye thamani ya Sh.100, 000.

Waliiba pia, televisheni moja yenye thamani ya Sh.1, 200,000 mali ya Denis Elirehema Swai na wakati huo huo kuwaweka chini ya ulinzi, Idda Denis Swai na Daniel Shayo na kuchukua mali hizo.

Wakati kosa la pili linalowakabili ni kukutwa na mali inayosadikika kuwa ya wizi ambayo ni kinyume na Kifungu 312 (1) (b) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Mwaka 2019.

Katika ushahidi wake, mkaguzi huyo wa polisi, alidai kuwa mshtakiwa wa kwanza (Mwaipopo), alikamatwa na maofisa wa polisi katika Kituo cha Mabasi cha Bomang'ombe, Wilaya ya Hai, Januari 25 mwaka 2018 akiwa na silaha, aliwaeleza makachero wa polisi kwamba iko Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha.

Aliendelea kudai kuwa, Machi Mosi mwaka 2018, walianza safari kwenda kuitafuta iliko silaha hiyo na waliikuta ikiwa kwenye begi la mshtakiwa wa kwanza kwenye chumba alichopewa na shemeji yake, Ritha Godliving Makule.

Aidha alidai kuwa walipofanya upekuzi waligundua kuwa bastola hiyo yenye usajili 47012895, yenye rangi nyeusi haikuwa na magazine (kifaa kinachohifadhi risasi).

Wakati mshtakiwa wa pili, Fredrick Mkwembe (Samora White), yeye alikamatwa Januari 27 mwaka 2018 akiwa katika shughuli zake za bodaboda eneo la Bonite, Moshi.

Baada ya kutoa ushahidi huo, kuliibuka mabishano ya kisheria kati ya Mwaipopo na shahidi, huku Mwaipopo akitaka Mahakama iruhusu apewe maelezo ya shahidi huyo ili ayatumie kumhoji.

Baada ya mvutano huo na upande wa mashtaka kujibu mapingamizi hayo, Hakimu Mkuu Mkisi, aliahirisha kesi hiyo hadi Mei 6 mwaka huu.




Mkurugenzi wa Shirika la WaterAid Tanzania, Anna Mzinga (kulia), akikabidhi nyaraka za makabidhiano ya mradi wa maboresho ya chanzo cha maji cha Nangwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Hanang, mkoani Manyara, Almishi Issa, baada ya kukarabati miundombinu yake, katika hafla iliyofanyika wilayani humo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasichana 156,834 kupata chanjo saratani mlango wa kizazi

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WASICHANA 156,834 wenye umri wa miaka tisa hadi 14 mkoani Manyara, wameingizwa rasmi katika mpango mahususi wa kinga dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi ili kuwakinga na vimelea vya ugojwa huo.

Jana, Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI mkoani hapa, Dk. Charles Shija, aliyasema hayo wakati akizungumza na Kamati ya Afya ya Msingi juu ya namna serikali ilivyojipanga kuendesha kampeni hiyo.

Alisema chanjo hiyo itaanza kutolewa Aprili 22 mpaka Aprili 28 mwaka huu.

Alisema: "Tayari dozi 173,600 zimeishapokelewa mkoani pamoja na mabomba ya sindano 299,200 yanaendelea kusambazwa. Chanjo hiyo ilikuwa inatolewa kwa watoto wa miaka 14 mara mbili kila baada ya miezi sita, ila kwa sasa imeonekana chanjo ikitolewa mara moja inatosha kumkinga mtoto".

Vilevile, alisema kwa shule zilizoko karibu na vituo vya afya, watoto wataenda kuchanjwa, ila ambao vituo vya afya viko mbali, wataongozana na walimu kwenda vituo vya afya kuchanjwa.

Akizifafanua zaidi kuhusiana na chanjo hiyo, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Dk. Damas Kayera, alisema chanjo hiyo ilianza kutolewa mwaka 2018 na mwaka jana walitoa chanjo hiyo kwa asilimia 100 kwa awamu zote mbili.

Dk. Kayera, alisema kuwa chanjo hiyo imeboreshwa zaidi na sasa inaanza kutolewa dozi moja badala ya dozi mbili zilizokuwa zinatolewa awali.

Katika kikao hicho, Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange, alisema ili kufanikisha zoezi hilo watatumia viongozi wa dini, viongozi wa kimila na viongozi wa mitaa, vijiji na kata kufanya vikao na mikutano ya hadhara ili kutoa ujumbe kwa wananchi.

# Elimu ya fedha kufundishwa shule ya msingi, vyuo vikuu

**Na Gwamaka Alipipi**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wanatarajia kutoa elimu ya fedha kuanzia elimu ya msingi hadi vyuo vikuu.

Lengo likiwa ni kuwawezesha vijana kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha na kufahamu namna ya kuzitunza.

Akizungumza jana jijini Dar es salaam wakati akifungua warsha kuhusu uchopekaji wa elimu ya fedha katika mitaala ya elimu ya juu, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga alisema serikali imedhamiria kujenga uelewa wa masuala ya fedha kwa jamii.

Alisema BoT itaendelea kusimama na vyuo na taasisi za elimu na Wizara ya Elimu katika kuhakikisha dhana ya elimu hiyo inakuwa endelevu na inafundishwa katika ngazi za jamii.Aidha, aliviagiza vyuo vikuu kushirikiana na BoT kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango huo ili kuboresha mbinu na nyenzo za kufikisha ujumbe huo kwa jamii.

Naibu Gavana wa BoT, Sauda Msemo alisema elimu ya fedha inakuwa ni sehemu ya masomo itakayofundishwa ngazi zote kuanzia elimu ya msingi hadi vyuo vikuu.

Alisema: "Aprili mwaka jana BoT iliwashirikisha wakuu wa taasisi za elimu ya juu nchini, kwa uwakilishi wa wakuu wa vyuo vikuu pamoja na TCU na NACTIVET kwa lengo la kukubaliana juu ya azma ya kufundisha somo la elimu ya fedha ngazi ya elimu ya juu nchini".

Aliongeza: "Hadi sasa taasisi tatu za elimu ya juu zimechukua hatua za kuingiza somo la elimu ya fedha katika mitaala yao, hivyo warsha hii itachochea uwepo wa elimu ya fedha kwa vyuo vingi nchini kuendana na mabadiliko ya mageuzi ya kiuchumi nchini"

Sauda alisema takwimu ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 inaonesha asilimia 34.5 ya Watanzania ni vijana walio na umri kati ya miaka 15-35.

Alisema ili kuleta tija na ufanisi katika masuala ya uchumi ujuzi na uzoefu wa masuala ya fedha ni moja ya sifa muhimu kufikia azma hiyo.

Alisema elimu ya fedha kwa Watanzania itachochea maendeleo kwa kuongeza utumiaji rasmi wa huduma za fedha na kuwawezesha watu wengi kuwa na uwezo wa kufanya maamuzi sahihi ya kifedha na kuendesha shughuli zao kwa ufanisi na kukuza uchumi kwa ujumla.

Sauda alisema elimu kwa vijana wa vyuo vikuu itawasaidia kuweka akiba, kupanga bajeti na kufanya uamuzi wa masuala ya fedha kwa kuzingatia viashiria hatarishi na kuelewa taasisi mbalimbali zinazotoa huduma za fedha ili kufanya maamuzi sahihi ya fedha ili waitawale.

Pia, alisema BoT kwa kushirikiana na wadau wengine wa Baraza la Huduma Jumuishi za Fedha, imetoa mwongozo na mtaala wa elimu ya fedha kwa wakufunzi ambao utatumika na taasisi za elimu ya juu kwa kuwafundisha watoa huduma za elimu ya fedha kuwafikia wananchi.





# Monduli yakabiliwa uhaba madawati, vyoo

**Na Gwamaka Alipipi**

VIONGOZI na wananchi wa Wilaya ya Monduli, mkoani Arusha wameomba ushirikiano zaidi na Benki ya NMB kutokana na mchango mkubwa wa taasisi hiyo katika maendeleo yao na ujenzi wa taifa kwa ujumla.

Azma ya ushirika huo ilibainishwa jana katika Kata ya Meserani wakati benki hiyo ilipokabidhi madawati 130 yenye thamani Sh. milioni 15 kwa ajili ya shule tatu za msingi wilayani humo ambazo ni Sokoine, Ngalash na Olarash.

Wakizumgumza katika hafla ya makabidhiano ya samani hizo yaliyofanyika katika Shule ya Msingi Sokoine, wakazi hao walibainisha kuwa ushirikiano wao wa muda mrefu na NMB umekuwa wa tija na mafanikio makubwa kimaendeleo.

"Benki ya NMB imekuwa inajitoa sana kuisadia wilaya yetu, tunaomba ushirikiano huu uendelee na kudumishwa," Mgeni Rasmi, Kaimu Katibu Tawala wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, Anael Mbise, alisema katika hotuba yake. "Shule zetu bado zina uhitaji mkubwa wa vifaa yakiwamo madawati. Tunashukuru sana NMB kwa kuliona hilo na kuchangia madawati haya 130 mnayoyakabidhi leo," alisema kiongozi huyo aliyemwakilisha mkuu wa wilaya, Festo Kiswaga.

Diwani wa Meserani ambaye pia anaongoza Kamati ya Elimu ya Wilaya, Loth Tarakwa, alisema kwa sasa Monduli nzima inakabiliwa na upungufu wa madawati 1,114. Changamoto nyingine kubwa za elimu wilayani humo alizozitaja ni pamoja na kupungukiwa nyumba za walimu 282 na vyoo 887.

Meneja wa NMB Kanda ya Kaskazini, Ladislaus Baraka, alisema kwa miaka saba mfululizo benki hiyo imekuwa ikitenga asilimia moja ya faida baada ya kodi kwa ajili ya bajeti za kuwajibika kwa jamii (CSR).

Alibainisha kuwa pamoja na uwekezaji mkubwa inaoufanya serikali kuboresha maisha wa Watanzania, wao kama NMB wana wajibu mkubwa wa kusaidia kutatua changamoto zinazokabili jamii.

Aliongeza kuwa ushirikishwaji katika masuala ya maendeleo wanaoupata Monduli ni mfano mzuri wa ushirikiano wanaopewa kote nchini unaoifanya NMB kuongoza katika kujali na kujihusisha na masuala mbalimbali ya kijamii.

Ladislaus alisema huku akipongeza serikali kwa juhudi zake kubwa za kuiboresha sekta hiyo.

Ni katika muktadha huo, alifafanua Shule ya Msingi Sokoine imepata ufadhili wa madawati 50 sawa na Ngarash wakati Olar

Walimu wakuu wa shule hizo walisema mchango huo umepunguza uhaba wa madawati kwa kiasi kikubwa na kuwasihi wadau wengine kuinga mfano wa NMB katika hilo.

Mwalimu Abdallah Hoza wa Sokoine alisema kabla ya afua ya NMB, walikuwa na upungufu wa madawati 70 wakati Mwalimu Philipo Kadeghe alisema kuwa kwa Shule ya Msingi Olarash, tatizo limetatuliwa kabisa.

Mbunge wa Monduli, Fred Lowassa, alipongeza Benki ya NMB si tu kwa kusaidia kuweka mazingira rafiki ya kujifunzia na kufundishia Monduli, bali pia kwa ukaribu iliyonao na Watanzania wote, akisema mipango yake ya elimu ni endelevu hususani ufadhili wa masomo ya vyuo vikuu kupitia NMB Foundation.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita akikagua moja ya madarasa matano ya Shule ya Msingi Igwamanoni, kata ya Igwamanoni, Halmashauri ya Ushetu jana, yaliyotitia na kuleta nyufa kutokana na mvua za masika zinazoendelea kunyesha. Nyuma (kushoto) ni Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Hadija Kabojela na viongozi mbalimbali wa wilaya. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Katibu Mkuu Ardhi awafunda watumishi kuhusu migogoro

**Na Remmy Moka**, SAUT

WATUMISHI wa sekta ya ardhi wametakiwa kujiepusha kuwa chanzo cha kusababisha migogoro ya ardhi, bali wawe chachu ya kuleta maendeleo katika sekta hiyo.

Rai hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaz, Anthony Sanga wakati akizungumza na watumishi hao jijini Mwanza.

Alisema baadhi ya watumishi wamekuwa chanzo cha migogoro ya ardhi na kusababisha vilio kwa wananchi.

Hivyo, aliwataka watumishi hao kutenda haki wakati wa utatuzi wa migogoro ya ardhi na kutoitatua kwa kutazama watu wenye vipato, wasiwape haki ambayo hawakuistahili, bali watoe kwa yule anayestahili kupewa .

Aidha, aliwasisitiza kufuata sheria na kanuni na taratibu zilizowekwa katika utatuzi wa migogoro hiyo kwa kuzingatia hilo kutasaidia kuondoa matatizo hayo kwa urahisi kulinganisha na hapo awali.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Mwanza, Happiness Mtutwa alisema katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 sekta ya ardhi katika Mkoa wa Mwanza imekusanya zaidi ya Sh. bilioni sita, huku wakiwa wametatua matatizo zaidi ya 5,000 zinazohusiana na hati katika mkoa huo.

Alisema licha ya kuwa na matatizo mbalimbali katika utekelezaji wa utatuzi wa migogoro katika sekta ya ardhi mkoani Mwanza, lakini watatenda kazi kwa umoja ili kuhakikisha hali ya sekta ya ardhi ndani ya mkoa inakuwa salama

Alisema baadhi ya migogoro ya ardhi inasababishwa na wananchi kwa kutokuwa waaminifu katika utoaji wa taarifa kuhusiana na ardhi.

# TFRA yahimiza matumizi ya mbolea, kilimo cha kisasa

**Na Renatha Msungu,** KAGERA

MWENYEKITI wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dk. Anthony Diallo amewataka wakulima mkoani Kagera kujikita kwenye kilimo cha kisasa kwa kutumia mbolea, ili kuongeza tija ya uzalishaji kwenye mazao mbalimbali shambani. Alitoa wito huo wakati wa ziara ya kusikiliza na kutatua kero za wakulima na mawakala wa usambazaji wa mbolea za ruzuku wilayani Ngara. "Nia yetu kubwa ni kuwajengea wezo wa kiuchumi wakulima kwa kuongeza uzalishaji baada ya kutumia mbolea zitakazosaidia kuongeza tija kwenye uzalishaji" alisema Dk. Diallo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent aliwataka wakulima kuwekeza zaidi kwenye kupima afya ya udongo ili waweze kutumia mbolea inayoendana na uhitaji wa udongo. Alisema matumizi sahihi ya mbolea yanaleta tija kwenye uzalishaji, hivyo aliwasihi wakulima kuendelea kutumia mbolea sahihi kulingana na uhitaji wa udongo wao baada ya kuupima. Kaimu Meneja wa chama cha wakulima Ngara, Fadhili Damian Kamhanda alisema Wilaya ya Ngara ilifanikiwa kupokea tani 65 za mbolea sawa na mifuko 1,300 iliyosambazwa kwa wakulima kwa asilimia 98.

Alisema chama chao kiliingia mkataba na kampuni za OCP na Minjingu ili kusambaza mbolea za ruzuku ambapo ni mara ya kwanza kwa mbolea kufikishwa wilayani humo.



Ukurasa 12

UCHUMI BULUU, JINSIA NA BIDHAA DAGAA...

**Kinanama wajasiriamali wa Fungu Refu walivyoshikilia soko, wateja wakuu DRC**




Ukurasa 13

Wakuu mtumie yatokanayo kambi mafuriko, staili ya MBWA kuwajibika

BUFE

IJUMAA APRILI 19, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 14

**Ushirika yaingilia soko pamba, ikibeba wakulima kwa ubunifu 'malipo ya pili'**

MKUU TIC AMWAGIA SIFA RAIS...

# Sheria, sera mpya zimewawezesha kuvunja rekodi miradi mipya

- Ziara na semina zinavyovuna wawekezaji
- Mitaji 1000 yaja; nje Dola Bn. 5, nchini 3.5,

**Na Joseph Mwendapole**

HADI sasa serikali ya Awamu ya Sita ilipoingia madarakani mwaka 2021, moja ya eneo la jitihada zake ilikuwa kuvutia uwekezaji wa nje na ndani, kwa kuandaa mazingira mazuri yaliyovutia wawekezaji wengi kumiminika nchini.

Hilo limefanyika tangu mwaka huo na mpaka sasa Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC), ndicho kimepewa jukumu hilo, ambacho pia ni sehemu ya wajibu wake tangu kuundwa.

Sasa, kinajivuna kwamba 'kimeweka historia ya aina yake' kwa maelezo tangu kuanzishwa hakijapata kufikia rekodi tajwa, kutokana na kusajili miradi mingi kwa kipindi kifupi cha miaka mitatu jumla yake ni 1,188 yenye thamani ya Sh. trilioni 38.3.

Mkurugenzi Mkuu wa TIC, Gilead Teri, anawaelezea waandishi wa habari, namna ya uwajibikaji wake unavyoitikia usimamizi wa mkuu wa nchi katika miaka mitatu sasa wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Anafafanua kuwa, katika eneo la uwekezaji ni kwamba kuna mwitikio mkubwa kihistoria katika mfumo wa kisera na miongozo ya Rais Dk. Samia, sasa wawekezaji wanazidi kumiminika nchini, ikitajwa wanavutiwa na mazingira mazuri aliyoyaweka.

Teri anasema, kati ya miradi hiyo iliyosajiliwa asilimia 35 inamilikiwa na Watanzania, asilimia 41 na wageni na asilimia 24 ni ya ubia kati ya Watanzania na wageni.

Anasema kuanzia Machi 2021 hadi mwaka huu, TIC imesajili jumla ya miradi 1,188 sawa na ongezeko la asilimia 63.19, ikilinganishwa na miradi 728 iliyosajiliwa katika kipindi kama hicho, Machi 2018 hadi Machi 10, 2021.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akizindua mradi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

### AJIRA VS MIRADI

Teri anaeleza kuwa, katika ajira zilizozalishwa kutokana na usajili wa miradi, kumekuwapo ongezeko la asilimia 231.63.

Anafafanua kwamba kulikuwapo ongezeko la ajira 104,172 zilizozalishwa katika kipindi cha miaka mitatu, kati ya mwaka 2018 mpaka 2021.

Lakini kwa sasa, Teri anasema kiwango kama hicho kinaongezeka kufika ajira 345,464, kwa hesabu inayotarajiwa kwa ajira mpya kati ya Machi 2021 mpaka Machi mwaka huu.

Anasema, pia kumekuwapo ongezeko la usajili wa miradi kutoka nje linatokana na juhudi zinazofanywa na Rais Samia katika kuitangaza nchi na kuhamasisha uwekezaji kupitia, Sera Maalum ya Ushirikano kupitia diplomasia ya kiuchumi.

Anasema ongezeko hilo la miradi linatokana na ushiriki wa Tanzania katika makongamano mbalimbali nje ya nchi na maboresho mbalimbali, yanayofanywa na serikali kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kupitia Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini

Teri anasema, tathmini inaonyesha idadi kubwa ya miradi iliyosajiliwa ipo katika sekta za kipaumbele ambazo; uzalishaji viwandani miradi 538, usafirishaji miradi 225; utalii miradi 110; ujenzi wa majengo ya biashara miradi 106; na kilimo miradi 106.

Pia, ansema Tanzania inaendelea kuwa kinara Afrika Mashariki katika kupokea wawekezaji wenye nia ya kuwekeza nchini na kwamba hiyo imetokana na mabadiliko yaliyofanywa kwa kuleta sheria mpya na bora ya uwekezaji ya Tanzania ya mwaka 2022.

Mkurugenzi huyo anasema, Sheria za Uwekezaji zina nafasi muhimu katika kuboresha mazingira ya biashara na kuchagiza wawekezaji. kwani imevutia uwekezaji wa moja kwa moja (FDI) zaidi nchini Tanzania.

Anasema, vivutio vya kodi na sheria mpya za uwekezaji zinatoa vivutio mbalimbali vya kodi na visivyokuwa vya kodi, ili kuhamasisha uwekezaji wa ndani na wa kigeni na kwamba vivutio hivyo vinajumuisha vivutio vya kodi kwa wawekezaji wa kawaida na wa kimkakati.

**INAENDELEA UK.14**


BIASHARA

UCHUMI BULUU, JINSIA NA BIDHAA DAGAA...

# Kinanama wajasiriamali wa Fungu Refu walivyoshikilia soko, wateja wakuu DRC

• Kiwanda kiko mbioni; uzalishaji visiwani wapaa 210%

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR



LICHA ya Zanzibar kuwa na utajiri mkubwa wa uvuvi, inatajwa bahari yake inapotumiwa vizuri, kuna maendeleo makubwa yatapatikana, kwa kupitia fursa zilizomo baharini na Ukanda wa Pwani.

Uvuvi unatajwa kuwa muhimu kwa maendeleo ya jamii katika maeneo yanayopakana na maji. Pia, ili sekta hizo kuleta tija, inapaswa kutumia teknolojia za kisasa na ushirikishwaji sekta binafsi.

Ni sababu ambazo visiwa hivo sasa, vinasifika kwa biashara ya usafirishaji dagaa kavu, penye soko kubwa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Kuna eneo tajwa la Fungu Refu, kisiwani Unguja maarufu kwa shughuli za uvuvi, ukaushaji na uanikaji dagaa, kabla ya kuingia sokoni kuuzwa.

Hapo kuna wafanyabiashara wengi watokao nchi jirani ya DRC, wakifuatilia soko la dagaa hao, Kaskazini mwa Unguja.

Eneo hilo limekusanya wajasiriamali zaidi ya 2000 wanaofanya biashara hiyo ya dagaa kutoka maeneo mbalimbali ya visiwa vya Unguja, Pemba na baadhi ya mikoa ya Tanzania Bara, ikiwamo Tanga, asilimia 80 ya wanaoshughulika ni kinamama.

### MWENYEKITI GRACE

Grace Ngoti (39), ni miongoni mwa wajasiriamali hao anayesema eneo hilo ndilo tegemeo kwake na kinamama wenzake katika kukuza kipato chake na kuendeleza familia kupata mahitaji muhimu, ikiwamo chakula na kusomesha watoto wake.

Anasema, ni zaidi ya miaka 10 sasa anafanya biashara hiyo ya kuanika dagaa, akinunua kutoka kwa wavuvi, anapika na kulikausha kwa jua kabla ya kuwauza.

Grace, mama wa watoto watatu, yuko na kinamama wenzake wengi akiwaongoza katika nafasi yake ya Mwenyekiti wa Wajasiriamali Wanawake, katika eneo hilo.

Anasema, ili kukuza biashara yao hiyo ambayo ni tegemeo anashauri imefika wakati serikali ikawajengea uwezo, kwa kuwapatia mtaji na kuacha kutegemea matajiri wateja wa kigeni, ambao 'huwalazia'' katika kununua dagaa.

Anasema mjasiriamali anapopata mtaji mzuri, anafanya biashara vizuri, ikiwamo kununua dagaa na kuwasafirisha nje ya nchi, kwa sababu soko la uhakika lipo.

> **"Kwa sasa hatuna mtaji wa kutosha wa kufanya biashara hii na matokeo yake tunategemea matajiri kutoka Congo (DRC) ambao ndiyo wanaotupangia bei ya kununua dagaa.**

### WANAVYOLALIWA SOKONI

Mwenyekiti huyo anasimulia, wanachokifanya matajiri wao kutoka DRC huwapa fedha na kutafuta dagaa ambazo baadaye hutaka wauziwe kwa bei wanayoitaka wao, bila ya kujali gharama na muda alioupoteza mjasiriamali.

''Kwa sasa hatuna mtaji wa kutosha wa kufanya biashara hii na matokeo yake tunategemea matajiri kutoka Congo (DRC) ambao ndiyo wanaotupangia bei ya kununua dagaa,''anasema.

Mjasiriamali Fatma Haji Juma (41), anasema kilio chao kikubwa ni serikali kuwezesha ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa katika eneo hilo, ambacho kitaongeza thamani ya bidhaa hiyo kuwa na matumizi mengi zaidi.

Anasema ujenzi wa kiwanda, ndiyo mkombozi kwao na kitaleta mageuzi makubwa katika biashara yao na serikali ikipata kodi.

''Tunaamini biashara hii itakuwa mkombozi kwetu na kufika wakati wa kuacha kutegemea soko moja la Congo,''anasema.

Katibu wa Umoja wa Waanika Dagaa katika eneo hilo la Fungu Refu, Mkubwa Fundi Kombo, anasema serikali inawafahamu wafanyabiashara wa eneo hilo, kwa sababu kupitia mamlaka husika, hukusanya kodi kutoka kwao.

''Biashara ya kuanika dagaa katika eneo la Fungu Refu ni maarufu. Hivi sasa asilimia 80 inafanywa na wanawake ambao wameonyesha utayari katika kujikomboa, pamoja na kushiriki kikamilifu katika Uchumi wa Buluu,'' anasema.

Rai yake serikali anaitaka iwajengee kituo kidogo cha polisi, kwa sababu kuna mkusanyiko mkubwa wa watu, hivyo hata pakitokea uhalifu, inakuwa rahisi kuwafikia, badala ya kutegemea huduma ya mbali Mkokotoni.



Mjasiriamali Grace Ngoti akizungumza na waandishi wa habari waliofika katika eneo la Fungu Refu, Kaskazini Unguja eneo ambalo ni maarufu Zanzibar kwa biashara ya dagaa.

Mjasiriamali, Fatma Haji, akianika dagaa kabla ya kwenda sokoni katika eneo la Fungu Refu, Kaskazini Unguja. **PICHA ZOTE: RAHMA SULEIMAN**

### WADAU WA KINAMAMA

Ofisa Mradi wa Wanawake na Uongozi katika Siasa na Uchumi, kutoka katika Chama cha Waandishi wa habari Wanawake Tanzania (TAMWA) - Zanzibar, Mariyam Ame Chum, anasema shughuli za kiuchumi zinazofanywa na wanawake wa Fungu Refu, zinahitaji kuungwa mkono, ili wanawake wafikie malengo ya kujitegemea kiuchumi.

Anaitaka Hamlashauri ya Mkoa husika, kupaimarisha Fungu Refu, ikiwamo ulinzi na usalama kwa wajasiriamali wanawake, hatua inayowaongezea ufanisi wa kufanyika kazi bila ya hofu.

''Mradi wa Wanawake na Uongozi katika Siasa na Uchumi (SWILL), ambao unafadhiliwa na serikali ya Norway, umefurahishwa na juhudi zinazochukuliwa na wajasiriamali waliopo Fungu Refu ambao kwa asilimia 80 ni wanawake, wanavyojituma katika kujiimarisha kiuchumi na kujitegemea" anatamka Maryam.

### KIWANDA CHAJA

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, inatarajia kuingiza mamilioni ya fedha, baada ya kukamilika ujenzi wa Kiwanda cha Kusarifu Dagaa kinachoendelea kujengwa katika wilaya ya Magharib A, Unguja.

Matarajio yaliyopo yanatajwa kuwa kiwanda hicho kuwa na uwezo wa kuzalisha tani 20 za dagaa kavu kwa siku, zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 200. Hadi sasa dagaa ni sehemu ya mazao makuu ya kimkakati visiwani humo, katika sekta ya uvuvi na mazao ya baharini, sasa mipango iliyoko ni kuliinua zao hilo kupitia ushindani wa kisiasa kwa ubora masokoni, ndani na nje ya nchi.

### HALI YA UZALISHAJI

Aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi (sasa yuko Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale), Aboud Suleiman Jumbe, anasema Zanzibar chini ya uongozi wa Rais Dk. Hussein Mwinyi, uzalishaji dagaa umeongezeka.

Jumbe anafafanua kuwa takwimu inabadilika, kwa nyongeza kutoka tani 2,405 zenye thamani ya shilingi bilioni 10.33 hadi tani 21,827 zenye thamani ya shilingi bilioni 89.31.

Anasema, pia usafirishaji wa dagaa umeongezeka kutoka tani 3,579 zenye thamani ya shilingi bilioni 12.31 mwaka 2020, hadi kufikia wastani wa tani 9000 zenye thamani ya milioni 35 kwa mwaka 2023.

Anataja mafanikio ya uzalishaji dagaa, yamewezesha kutanuka sekta ya uvuvi wa samaki kutoka tani 38,107 mwaka 2020 hadi tani 80,085 zenye thamani ya shilingi bilioni 569.08 kwa mwaka huu. Ni ongzeko la asilimia 210.

"Ongezeko hilo ni ushihidi mkubwa wa kihistoria na imewezesha wavuvi kupata ajira na kuinua hali zao za maisha.

"Takwimu za hivi karibuni zinaonyesha kuendelea kukua kwa kasi kubwa kwa sekta ya uvuvi nchini kwa kiwango cha asilimia tisa kwa mwaka," anasema Jumbe.

Pia, anafafanua mchango wa sekta ya uvuvi katika Uchumi wa Buluu umeongezeka kufika wastani asilima 17.40, matarajio ya kuwapo kiwanda cha kukausha dagaa, kitachochea ongezeko la mapato yao, kutoka shilingi 435,300 za sasa, hadi shilingi 742,500 kwa mwezi.

Sensa ya mwisho ya uvuvi mwaka 2020, inataja Zanzibar kuwa na wavuvi 88,000, huku asilimia sasa ikifafanuliwa kimaisha asilimia 21 ya Wazanzibari wanatumikia Uchumi wa Buluu.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) Amiri Haidar Mshenga, anasema mradi huo wa kujenga miundombinu ya dagaa, ni miongoni mwa utekelezaji wa ahadi zake Rais Dk. Mwinyi, kwa wajasiriamali wanaosarifu dagaa.

Mshenga anasema, Zanzibar ina wastani wa wajasiriamali 16,000 wa dagaa, Unguja wakiwapo 14,000 na 12,000 Pemba.

Vilevile, kuna jumla maeneo matatu yametengwa kwa ajili ya mradi wa usarifu wa dagaa, ikiwamo Fungu Refu na Ndagoni.

Anasema, mradi huo unatarajiwa kujumuisha ujenzi wa viwanda viwili vya kusarifu dagaa, ujenzi wa majengo ya kuoshea dagaa, majengo ya kuchemshia dagaa, jengo la mtambo baridi kwa ajili ya kuhifadhia dagaa na mtambo wa kuzalisha barafu na jengo la biashara.

"Hadi kukamilika kwa kiwanda hiki, sisi ZAFICO tutaweka chanja 5000 za kuanikia dagaa na mradi huo kwa awamu ya kwanza utakamilika mwaka huu na unatarajiwa kuajiri wajasiriamali zaidi ya 10,000 wakiwamo wavuvi na wafanyakazi wa sekta ya dagaa," anaeleza.

### HIFADHI MAZAO BAHARI

Mkurugenzi wa Idara ya Uhifadhi wa Mazao ya Baharini, Dk.Makame Omar Makame, anasema mikopo tayari imeshatolewa kwa awamu mbili tofauti, kwa sasa wanasubiri kadri fedha zitakazorejeshwa, ili kuwapatia wengine.

Anasema, Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini, miongoni mwa majukumu yake ni kuratibu wajasiriamali wanaofanya kazi za uzalishaji dagaa, wakiwamo wa Fungu Refu Mkoa wa Kaskazini Unguja, kuona namna wanavyofanya shughuli zao kwa mafanikio makubwa.

Anasema, Kiwanda cha Kusarifu Dagaa, kwa kiasi kikubwa kitawafanya wajasiriamali hao, kufanya shughuli zao kitaalamu zaidi kwa kutumia teknolojia ya kisasa, ikianzia wanavyowaanika dagaa.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Wakuu mtumie yatokanayo kambi mafuriko, staili ya MBWA kuwajibika






**NA PETER ORWA**

MARA zote katika taaluma na majukumu ya kikazi, inapotokea dharura ya ama mazuri au mabaya, mhusika mkuu huwa anakumbuka wajibu wake wa msingi.

Mwanafunzi, hali kadhalika mwalimu wake anaposikia msamiati 'mtihani' daima wanabadilika ghafla kujiweka tayari kukabili kijacho.

Kanuni zote za kitaaluma hurejeshwa haraka kumbukumbu mahsusi kwa somo tajwa na kujinoa kusikoisha huchukua nafasi yake. Maana hata Mjerumani Dikteta Addolf Hitler, aliyeaminika haogopi chochote duniani ikiwamo kifo, inadaiwa alipohojiwa akasema anachokiogopa maishani mwake ni mtihani pekee.

Dharura hiyo na mandalizi ya staili hiyo ndio anayo hata mkulima, mfanyabiashara kwa soko jipya au askari ambaye anarejea kuwa 'soja' akiweka silaha yake 'haipoti', inaanzia katika dharura ya usalama.

Baada ya hayo kupita, kitaaluma hufanyika majumuisho au tathmini za staili mbalimbali, lengo ni kujifunza kulikopatiwa na kulikosewa kwa ajili ya waendako.

Kwa wanahabari na wenzao wengi wanaangukia majukumu ya kitaaluma, huingia katika tahmmini ya kina pamoja baadaye kuumiza vichwa, inayoitwa 'postmortem', kama ilivyo kwa madaktari kutafakari kazi zao.

Sasa ikiangaliwa kitaifa kuna dharura ya mfuriko tarkiban mikoa sita; kuanzia na Rufiji mkoani Pwani, Kilombero (Morogoro), Geita, Arusha, Mbeya ma Mwanza mvua imezalisha mafuriko makubwa, hali kama hiyo ikitokea hata nje ya mipaka kama kwa majirani Beira Msumbiji na huko Uarabuni.

Mara moja, uongozi wa juu wa nchi umeagiza wakuu wa kiserikali, wakiongozwa na mawaziri kupiga kambi kuwajibikia kusaidia waathirika.

Ni sentesi kubwa na nzito sana, kutoka kwa mkuu wa nchi. Mosi, ni ishara ya walioko juu wanawawajibikiaje walio chini.

Lakini, kuna la pili hapo kupitia 'postmortem' zao wakubwa hao, hawatakiwi kuwasahau waathirika baada ya kuwawajibikia misaada hiyo katika kipindi cha dharura kilichoko.

Bado tunakumbuka marais Dk. Samia Suluhu Hassan, mtangulizi wake hayati Dk. John Magufuli na watangulizi wao, wamekuwa wakisisitiza wajibu viongozi kwenda waliko wananchi kutambua shida zao na kuzifanyia kazi wakiziona.

Ni hivi karibuni, Rais Dk. Samia akawakumbusha mawaziri, huku akitoa mfano wa anayetumia staili hiyo na kumpa kongole, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Slaa, anavyowezesha kumaliza kero za ardhi papo kwa hapo, kupitia ziara hizo.

Sasa mtambue mawaziri, hilo la kuweka kambi linapswa kuwa staili ya kudumu katika kufanikisha kilichomo kwenye hadidu za rejea za majukumu yenu.

Ile timu inayoweka kambi naamini mtakuwa na safari za kutosha kuifuatilia huko kote penye majanga, maana hata msimamizi mkuu wa serikali, Waziri Mkuu wiki hii tukamshuhudia analitenda hilo akiwa angani anakagua kwa helikopta kinachojiri katika mafuriko ya Morogoro.

Utendaji huo ni tiba, unaopotekelezwa kwa usafaha na wasimamizi wakuu wa ngazi mbalimbali, kama vile wakuu wa mikoa na wilaya una maana kubwa.

Ni uwajibikaji wa majukumu, pia kwa umma ambao ndio mabosi wenu wakuu, ikiwa sehemu ya staili ya menejimenti na utawala, ambao watafiti tangu zama hizo walikuna vichwa na kuja na nadharia inayohubiri hilo.

Wenyewe wanaiita nadharia ya MBWA, kwa maana yake kizungu 'Management By Walking Around' akimaanisha staili ya menjimenti, mkuu akifanya usimamizi kujua kinachoendelea katika picha halisi huko huko kunakohusika.

Ni wiki iliyopita katika kumbukumbu ya kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu Edward Moringe Sokoine, mengi yalisimuliwa kifo chake kilitokea akiwa safarini kutoka Dodoma Kwenda Dar es Salaam, akitumia fursa hiyo kukagua hali halisi ya mandeleo ya kilimo, badala ya kutumia ndege. Kimsingi, akiwa kiongozi alikuwa anatekeleza nadharia ya MBWA katika majukumu yake.

**• Mwandishi wa safu hii wiki hii amekosekana kwa sababu zisizozuilika. Mhariri.**

BIASHARA

# Ushirika yaingilia soko pamba, ikibeba wakulima kwa ubunifu 'malipo ya pili'

## • 'Yafunika' wanunuzi binafsi, uzalishaji ghafla wapaa

**Na Shaban Njia, KAHAMA.**

KATIKA Kanda ya Ziwa, zao la pamba linashika nafasi kutetea maisha yao kiuchumi, ikiwa ni zao la biashara.

Walioko shambani ni wakulima wadogo, ambao mchango wao unategemewa zaidi kuleta mageuzi, wakimiliki mashamba ukubwa kuanzia ekari moja, hadi 10.

Aidha, wakulima hao wanakaodiriwa kufikia 600,000 nchini wametapakaa katika mikoa takribani 17, katika Kanda mbili; Magharibi na Mashariki. Wengi wanalima mazao mchanganyiko kujiongezea kipato na chakula kifamilia.

Pamba inayolimwa Tanzania, inategemea zaidi soko la nje kwa asilimia 60 na asilimia 40 kwa viwanda vya ndani. Inatajwa sokoni inahitajiwa sana, kuliko kiwango cha uzalishaji uliopo, kwa sasa unafika marobota 300,000 pekee.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme (katikati), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 128.304 kwa Mwenyekiti wa AMCOS ya Isanjabadugu Jumanne Gwesa, kuwalipa wakulima wa pamba wa Ushetu, Msalala na Manispaa ya Kahama, waliokiuzia pamba Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU). **PICHA: SHABAN NJIA**

### KACU KWENYE USHINDANI

Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) kwa kuona umuhimu huo, kimeingia kwenye ushindani wa kununua pamba, kuchakata na kuuza nyuzi zake dhidi ya kampuni nyinginezo.

KACU ilianza hatua hizo kwa mtindo wake kimasoko 'malipo ya kwanza na pili'. Mara ya kwanza msimu wa kilimo 2019/2020, ambao kila kilo ililipa Sh.40 na zaidi ya Sh. milioni 90 zilitumika kwa malipo, hasa kutoka wilaya za: Kahama na Kishapu mkoani Shinyanga, pia Nyang'hwale mkoani Geita.

### USHIRIKA KACU

Mwenyekiti wa Bodi ya KACU, Tano Nsabi, anasema kuna zaidi ya wakulima 1000 wanaolima mazao mchanganyiko ya chakula na biashara, ikiwamo pamba katika halmashauri za Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama.

Pia, wanahakikisha mbolea na pembejeo zinawafikia kwa wakati kulingana na majira yake.

Anasema, ongezeko la uzalishaji pamba umekuwa ukitegemea. Hata hivyo anasema, kunapokuwapo mvua nyingi, zao hilo hushidwa kuchanua kupata pamba za kutosha.

Nsabi anasema ni hatua inayolenga kuwafanya kuweka ushindani wa bei na kampuni nyingine, pia, wakiwawezesha wakulima kuzalishe zaidi.

Anasema fedha zinazotumika kununua mazao, zinatokana na mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

Pia, anataja msimu wa kilimo 2023/2024, walikopa shilingi bilioni tisa na kununua jumla ya kilo milioni sita za pamba mbegu.

Hivyo, anasema baada ya uchambuaji pamba kukamilika, wamefanikiwa kuzalisha marobota 10,608 za nyuzi zenye uzito kilo 1,959,715 na kilo 2,891,260 za mbegu.

Kwa maana hiyo, anasema wamebakiza kilo 6,038 za pamba mbegu ambazo hazijachambuliwa, kwa ajili ya majaribio ya mitambo kwa msimu ujao.

### MALIPO YA PILI

Nsabi anasema, malipo ya pili yameanza kutolewa tangu msimu wa kilimo wa 2020/2021 kwa kutolewa shilingi milioni 90.9 na faida iliyopatikana baada ya kununua na kuuza pamba nyuzi na mbegu, baada ya kuichakata katika kiwanda chao, mwaka huo walilipa shilingi 40 kwa kila kilo moja.

Anasema, msimu huo walinufaika wakulima kutoka Wilaya ya Kishapu, Msalala, Ushetu, Manispaa ya Kahama na Nyang'hwale wa moa jirani, Geita. Kuna kilo milioni 2.2 zilinunuliwa na shilingi bilioni 2.049 zilitumika kununua pamba kwa wakulima.

Aidha anasema, katika milioni 90 iliyotolewa wakulima wa Kishapu walipata milioni 56.071 sawa na kilo Milioni 1.4, Msalala milioni 3.2 sawa na kilo 82,045, Ushetu milioni 23.9 sawa na kilo 598,435, Manispaa ya Kahama milioni 1.003 sawa na kilo 25,091 na Nyang'hwale Mkoani Geita milioni 6.6 sawa na kilo 166,300.

Nsabi anasema, msimu huu wa 2023/2024 wamelipa malipo haya kwa wakulima waliokiuzia chama kikuu cha ushirika(KACU) pamba kiasi cha Sh.milioni 186,316,776 hali iliyosaidia kuongeza uzalishaji na ushindani wa bei na makampuni mengine yanayonunua zao hilo

Aidha malipo hayo yametolewa kwa wakulima wa Halmashauri za Msalala, Ushetu, Kishapu na Manispaa ya Kahama na kulipwa Sh.36 kwa kila kilo moja na wale waliouza pamba yao kwenye makampuni mengine wanakosa nafasi hii.

Kadhalika, wakulima wa ushetu wamelipwa milioni 113,843,016 sawa na kilo milioni 3,162,306, Msalala kilo 241,760 sawa na Sh.milioni 8,703,360, Manispaa ya Kahama kilo 159,960 sawa na Sh.milioni 5.758,560 huku wakulima wa kishapu wakiuza kilo milioni 1,611,440 sawa na Sh.milioni 58,011,840.

Anasema wakulima walikiuzia chama pamba mbegu kilo milioni 5,175,466 na baada ya kuchakata na kuuza, wamewalipa sehemu ya faida shilingio.36 kwa kila kilo moja sawa na milioni 186.3, watakaotumia kuandaa msimu ujao 2024/2025.

### USHINDANI BEI

Meneja wa pamba wa KACU, Amiri Mwinyimkuu, anasema kwa kipindi cha miaka minne mfululizo, wamekuwa na ushindani mkubwa wa bei ya zao hilo, dhidi ya kampuni nyingine.

Anafafanua, katika msimu 2019/2020, bei elekezi iliyoetolewa na serikali ilikuwa Sh. 8,010 kwa kilo, ila wao wakainunua kwa Sh.9020.

Mwinyimkuu anasema, kwa msimu uliofuata 2021/2022 walinunua pamba kilo milioni 3.469 kwa bei shilingi 1,456, huku bei elekezi ya serikali ikiwa shilingi 1,825.

# Sheria, sera mpya zimewawezesha kuvunja rekodi miradi mipya

**INATOKA UK.11**

MATARAJIO YAJAYO

Teri anasema, matarajio ya TIC kwa mwaka wa 2024, ni kusajili miradi 1,000 ya uwekezaji katika kipindi cha msimu wa 2024 na kuweka malengo ya kuvutia mitaji ya kigeni yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni tano na kuvutia mitaji ya ndani ya Dola za Marekani bilion 3.5.

Anasema TIC imejipanga kuhakikisha asilimia 10 ya miradi iliyosajiliwa, ikilenga katika kuchangia juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuonyesha jitihada za kituo hicho za kusukuma mbele uwekezaji wenye manufaa na endelevu.

Pia, anasema serikali imeweka kipaumbele katika kuvutia miradi ya ujenzi wa kongani za viwanda (Industrial Parks) ili kurahisisha na kuharakisha ujenzi wa viwanda, sambamba na kukabiliana na changamoto za ardhi kwa ajili ya uwekezaji, yenye miundombinu wezeshi.

Anasema TIC, imeweza kuvutia miradi mikubwa kama Sino Tan Industrial Park, Kamaka – Kibaha, Pwani, vyote vipo katika hatua ya ujenzi, pia kituo hicho kinaendelea kufanikisha uwekezaji wa Elsewedy kutoka Misri kuwekeza maeneo ya Kikongo mkoa wa Pwani.

Mkurugenzi huyo anasema TIC, pa imefanikiwa kuhamasisha na kuvutia uwekezaji kwa kuandaa makongamano ya uwekezaji. kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ikiandaa na kushiriki makongamano ndani na nje ya nchi.

Anasema, Tanzania inaendelea kuwa kinara Afrika Mashariki katika kupokea wawekezaji wenye nia ya kuwekeza nchini na kwamba ni hli inayotokana na mabadiliko yaliyofanywa, kwa kuleta sheria mpya na bora ya uwekezaji ya Tanzania ya mwaka 2022, yakiweza kuvutia uwekezaji zaidi nchini.

Anasema sheria za uwekezaji zina nafasi muhimu katika kuboresha mazingira ya biashara na kuchagiza wawekezaji. Hapa kuna sababu chache kwa nini Sheria Uwekezaji ya Tanzania, kuanzia mwaka 2022 imeweza kuvutia uwekezaji wa nje nchini Tanzania.

Teri anasema vivutio vya kikodi, sheria hiyp mpya za uwekezaji zinatoa vivutio mbalimbali vya kikodi na visivyokuwa vya kodi ili kuhamasisha uwekezaji wa ndani na wa kigeni na kwamba vivutio hivyo vinajumuisha vivutio vya kodi kwa wawekezaji wa kawaida na wa kimkakati.

# Tumbaku yaiingizia serikali mapato ya tril.1/-

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKURUGENZI Mkuu wa Bodi ya Tumbaku Tanzania (TTB), Stanley Mnozya amesema hadi Machi mwaka huu tumbaku imeliingizia taifa Dola za Marekani milioni 394 (Sh. trioni 1.018)

Amesema katika msimu wa mwaka 2022/23 zao hilo limeshika nafasi ya kwanza katika kuliingizia taifa mapato ya fedha za kigeni.

Alitoa takwimu hizo jana wakati wa mkutano wa mwaka 2024 ambao unawashirikisha washiriki kutoka mikoa inayozalisha tumbaku ambayo ni Iringa, Ruvuma, Katavi, Tabora, Kigoma, Shinyanga, Singida, Mara, Geita, Kagera, Morogoro na Mbeya.

Alisema tumbaku lina mchango mkubwa katika maendeleo ya nchini ambapo kutokana umuhimu huo mkubwa uliifanya serikali kutoa agizo la kuongezwa kwa uzalishaji wa zao hilo hadi kufikia kilo 200,000,000 ifikapo mwaka 2025.

Mnozya alisema hivi sasa mapato ya wakulima yameongezeka kutoka Sh. milioni 121.58 mwaka 2021/22 hadi kufikia Sh.milioni 401.5 mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 230.

Alisema mafanikio mengine yaliyopatikana ni kuongezeka kwa makusanyo ya ushuru wa halmashauri za wilaya kutoka Sh. bilioni 7.5 mwaka 2021/2022 hadi kufikia Sh.bilioni 21.5 mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 186.6.

Alisema mapato ya fedha za kigeni yameongezeka kutoka Dola za Marekani 186,639,238.57 mwaka 2022/23 hadi kufikia Dola za Marekani 394,452,618 15 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 112.5 ambayo ni kulingana na ripoti ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ya Machi 2024.

Mnozya alisema mafanikio mengine yaliyopatikana kutoka na tumbaku ni limechangia mapato zaidi ya Dola za Marekani 696,599,513 kwenye uchumi wa nchi kutokana na makusanyo mbalimbali ya zao kufikia Machi 2024 na ifikapo Juni 2024 litachangia mapato ya Dola za Marekani milioni 762.

Pia, alisema uzalishaji wa tumbaku umekuwa ukiongezeka ambapo katika msimu wa mwaka 2020/21 zilizalishwa kilo 58,507,937, mwaka 2021/22 kilo 60,874,831, mwaka 2022/23 kilo 122,858,564 na mwaka 2023/24 kuna matarajio ya kuzalisha kilo 178,521,508.

Kuhusu bei ya tumbaku, Mkurugenzi huyo alisema imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka akitolea mfano msimu wa mwaka 2020/21 tumbaku ya mvuke ilikuwa Dola za Marekani 1.62 hadi kufikia wastani wa Dola ya Marekani 2.33 msimu wa mwaka 2022/23, huku daraja la kwanza likiwa na bei ya Dola ya Marekani 3.2 kwa kilo moja.

Mkuu wa Wilaya ya Singida,Godwin Gondwe alisema serikali inatambua umuhimu wa zao hilo katika kukuza pato la taifa.




Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa Benki ya NBC, David Raymond (wa pili kushoto), akiwaonyesha wadau mbalimbali wakiwemo waandishi wa habari, gari aina ya BMW x1 itakayotolewa kwa mshindi wa kampeni ya akiba "Shinda Mechi Zako Kinamna Yako" ya benki hiyo, wakati wa uzinduzi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Majaliwa atoa maagizo 12 ukusanyaji maoni Dira ya Maendeleo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa ametoa maelekezo 12 kwa wakuu wa mikoa kukusanya maoni ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050, ambapo hadi Aprili mwaka huu zaidi ya Watanzania 623,914 wameshatia maoni yao kwa njia ya mtandao ikiwamo simu.

Akifungua semina ya viongozi hao iliyoratibiwa na Tume ya Mipango, Majaliwa aliwataka viongozi hao kutoa ushirikiano wa kutosha kwa timu za wataalamu zitakazotembea kwenye maeneo hayo, kukusanya maoni kwa njia ya mahojiano na wananchi. "Wakuu wote wa mikoa zingatieni kuandaa vikao na watendaji katika ngazi zote za utawala na kuwapa elimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo pamoja na umuhimu wake, nendeni mkasimamie na kuhakikisha zoezi la uhamasishaji wananchi kushiriki kutoa maoni linafanyika katika kila halmashauri katika mikoa yenu,"alisema. Kadhalika, aliwasihi viongozi wa dini kuhamasisha waumini wao kushiriki utoaji maoni katika diara hiyo, akiwaelekeza kuwasimamia watendaji walio chini yao kuandaa mikutano ya kuhamasisha wananchi kujitokeza kutoa maoni.

Kadhalika, aliagiza Wizara ya Mipango na Uwekezaji kuhakikisha makundi yote katika jamii yanafikiwa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia dira hiyo kuidhinishwa na Bunge kwa kuwa inayoisha haikuidhinishwa na chombo hicho. Alisema kati ya Watanzania 623,914 waliotoa maoni kwa njia ya mtandao hadi juzi asilimia 70 ni wanaume na wanawake ni asilimia 30, huku vijana wakiongoza kwa kutoa maoni ambapo asilimia 80 ya waliotoa maoni hadi sasa ni vijana wenye umri kati ya miaka 15-35.

# Jaji Mkuu: Vyuo vikuu kuzeni kliniki za sheria

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JAJI Mkuu, Prof. Ibrahim Hamis Juma amesema vyuo vikuu vinavyotoa elimu ya sheria nchini vinapaswa kukuza kliniki za sheria ili kupanua wigo wa upatikanaji wa haki kwa wananchi.

Akizungumza juzi kwenye Siku ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) iliyofanyika katika Shule Kuu ya Sheria, alisema msaada wa sheria ni huduma yenye umuhimu mkubwa, hivyo watoe elimu pana ya kumwezesha mwananchi wa kawaida kupata haki zake hata katika ofisi za umma.

Prof. Juma alisema kliniki za sheria zina faida kubwa kwa wanafunzi wanaotoa huduma kwakuwa zinawapa nafasi ya kujifunza.

Alisisitiza umuhimu wa elimu ya sheria kwa umma katika maeneo yenye shida hapa nchini ambayo ni pamoja na elimu ya uraia, katiba, uwajibikaji, unyanyasaji, ukatili wa kijinsia.

Alitaja maeneo mengine ni haki za mtoto na binadamu kwa ujumla, haki ardhi, migogoro ya ardhi, haki na ulinzi wa mlaji, mirathi, kuepuka matumizi mabaya ya mapingamizi mahakamani na matumizi ya sababu za kiufundi kuchelewesha haki, umuhimu wa kutumia njia za usuluhishi kutatua migogoro nje ya Mahakama na kusimamia maadili ya mawakili na watumishi wa umma.

# Wazazi watakiwa kutowaficha watoto wenye ulemavu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZAZI wanaoishi na watu wenye ulemavu wameshauriwa kutowaficha majumbani badala yake wawapeleke kwenye vyuo vya ufundi, ili kujipatia ujuzi utakaowasaidia kujitegemea na kuachana na kuomba.

Mkurugenzi Mkuu wa karakana ya utengenezaji wa vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu mkoani Dodoma, Mwita Marwa aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari akisema kuwaacha majumbani ni kuwatumikisha kama walinzi.

Alisema wakipata ujuzi huo kwenye vyuo hivyo vya ufundi pia utawawezesha kuondokana na maisha ya utegemezi wa kukaa barabarani na mitaani kuombaomba.

Alisema hivi sasa serikali imeridhia kutoa mikopo ya asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu ambayo haina riba.





# Kampuni za madini zaonywa kuajiri watoto migodini

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI mkoani Njombe imetoa onyo kwa kampuni za uchimbaji madini mkoani hapa kuepuka tabia ya kuwaajiri watoto.

Agizo hilo lilitolewa na Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omari wakati akifungua mafunzo kwa wadau na wachimbaji wa madini yaliyoandaliwa na Tume ya Madini mkoani hapa.

"Tuangalie ajira tunazotoa ziwe nzuri zenye manufaa na zenye faida kwa wote, tusiende tukatumie ajira kwa watoto haitakiwi. Kuna baadhi ya stori kwenye migodi baadhi inatumia watoto wadogo," alisema Omari.

Aidha, alitoa rai kwa wanawake mkoani hapa kuchangamkia fursa mbalimbali zinazopatikana kwenye migodi sambamba na kuingia ubia na kampuni ambazo zinavifaa vya kuchimbia.

Alisema sekta ya madini katika pato la taifa linachangia asilimia tisa kutoka asilimia nne kwa kipindi cha miaka ya nyuma.

Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa Njombe, Zabibu Napacho alisema katika Mkoa wa Njombe yapo madini ya kimkakati kama dhahabu, makaa ya mawe na shaba.

"Pamoja na shughuli za madini lakini Mkoa wa Njombe una leseni 400 lakini leseni ambazo zinafanya kazi ni 40 tu kwa hiyo tunahitaji kuendelea kutoa elimu na kuhamasisha ili kila mmiliki ajue wajibu wake," alisema Napacho. Alisema kuwa katika mkoa huo pia kuna ongezeko la makusanyo kuanzia mwaka wa fedha 2017 ambao tume imeanza kazi hadi mwaka 2024.

Alisema kwa mwaka wa fedha ulioanza Julai lengo la makusanyo lilikuwa Sh. bilioni 3.85 ambapo hadi sasa wamekusanya Sh. bilioni 3.5 sawa na asilimia 91.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, akikabidhi msaada wa fedha kiasi cha Sh. milioni 10 kwa waathirika wa maporomoko ya tope yaliyotokea hivi karibuni katika Kata ya Itezi, mkoani Mbeya na kufunika nyumba 20, alipowatembelea juzi. **PICHA: HALFANI CHUSI**

## Sababu watoto kufanyiwa ukatili Njombe zatajwa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MIGOGORO ya ndoa, imani za kishirikina na wazazi kutokuwa karibu na watoto wao ni miongoni mwa sababu zinazosababisha watoto kufanyiwa vitendo vya ukatili katika Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe.

Hayo yalibainishwa na Mwenyekiti wa Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii Tanzania (SMAUJATA) Mkoa wa Njombe, Giveen Tweve wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema kitendo cha wazazi kutengana kinasababisha watoto kukosa malezi bora na kushindwa kutoa taarifa pindi wanapofanyiwa ukatili.

"Watu wengi wamekuwa na elimu tofauti tofauti kwamba anaamini akifanya hivi au vile inakuwa hivi kwa hiyo kikubwa ni ukosefu wa elimu, suala la uchumi na changamoto nyingine ni suala la uhusiano na ndoa," alisema Tweve.

Katibu wa SMAUJATA, Athuman Chang'a alisema vitendo vya ukatili vinazidi kuongezeka hasa watoto wa kiume kulawitiwa na kueleza kuwa iko haja ya wazazi kuwa karibu na watoto wao, huku viongozi wa dini wakihimizwa kutoa elimu ya dini ili kukabiliana na vitendo hivyo.

Mwanasaikolojia kutoka Dawati la Jinsia na Watoto Kituo cha Polisi Makambako, Elpidius Mkandala alisema ili kukabiliana na vitendo vya ukatili katika jamii ni lazima wazazi watimize wajibu wao wa malezi na kuachana na unywaji pombe ulopitiliza.

# Serikali yagawa hekari 5,113 za Msitu wa Hifadhi ya Kuni

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SERIKALI wilayani Mvomero mkoani Morogoro imezindua ugawaji wa hekari 5,113 zilizoachiwa na serikali kwa wananchi katika Msitu wa Hifadhi ya Kuni eneo la Makunganya.

Eneo hilo awali liliwekwa zuio kwa muda wa mwaka mmoja kutoendelezwa baada ya kuvamiwa maeneo bila kufuatwa taratibu.

Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli aliyasema hayo wakati wa kikao cha Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na wananchi wa eneo hilo.

Judith alisema kufuatia maelekezo ya Serikali kupitia kamati ya mawaziri nane wa kisekta walipita kwenye eneo hilo wakati wa mgogoro huo Serikali imeamua kutoa viwanja hivyo kati ya eneo lililokuwa zaidi ya hekari 30,000 za msitu wa hifadhi unaomilikiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Nguli alisema upimaji wa viwanja hivyo umefanywa tangu mwaka jana ambapo tayari viwanja 14,000 vimeshapimwa na zoezi linaendelea kwa ajili ya kukamilisha viwanja 19,000 ambavyo vinapaswa kutolewa kwa wananchi.

Alisema zoezi la ugawaji viwanja hivyo litaanza baada ya wiki mbili kutoka kikao hicho ambapo wananchi watatakiwa kulipia ndani ya miezi sita kulingana na gharama zilizopangwa.

Aidha, aliwataka wananchi hao kuona umuhimu wa kulipa malipo ya viwanja hivyo kwa wakati bila kuwa na maombi mengine.

Pia, aliwaomba wananchi hao kulipa gharama kwenda sambamba na muda sababu wasipolipa kwenye muda watachukua hatua kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo ikiwemo kiwanja kugawiwa kwa mtu mwingine.

Hata hivyo, aliwahakikishia wananchi hao kutoona shida kulipa gharama za viwanja hivyo sababu eneo hilo tayari limeshapewa hadhi ya kuwa mji maarufu kwa kupewa jina la Suluhu New City.

Alisema eneo hilo linatarajiwa kuwekwa miundombinu yote muhimu ikiwemo shule, hospitali, soko, barabara na madaraja katika sehemu korofi na hivyo kupata wawekezaji na kukua kiuchumi kwa namna moja au nyingine.

Mtaalamu wa mipango na mambo ya ardhi kutoka Wizara ya Ardhi, Julius Mwakafwila alisema viwanja hivyo vimegawiwa katika kanda tatu. Alisema kanda ya kwanza ni kuanzia Barabara Kuu ya Morogoro -Dodoma hadi kulipokuwa kunafanyika mkutano awali ambako kutalipiwa mita moja ya mraba kwa Sh. 3000.

Mwakafilwa alisema kanda ya pili itakuwa kutoka walipokuwa wakifanyia mkutano awali hadi kwenye ghorofa ambao watalipa mita moja ya mraba Sh. 2000 na kutoka pale hadi mwisho watalipa kila mita moja ya mraba Sh. 1000.

Alisema kwa wale wenye nyumba na mapagala watalipwa Sh.2000 kwa mita moja ya mraba kuanzia wale wa barabarani hadi kwenye ghorofa, huku wale wa kutoka kwenye ghorofa hadi mwisho wakilipia Sh. 1000.

Baadhi ya wananchi wa maeneo hayo akiwemo Baraka Casbert alimuomba Rais Samia Suluhu Hassan kuwaongezea muda wa malipo na kupunguza gharama ya malipo kutoka Sh.2000 kwa mita moja ya mraba na kuwa Sh. 1000 hasa wale wenye nyumba kutokana na kuwa na kipato kidogo.

Moses Mtinde alisema awali walikumbwa na adha mbalimbali ikiwemo za kubomolewa nyumba, kwamba walishindwa hata kuzirekebisha baada ya kuwekewa zuio.





# Wakaguzi Afrika wavutiwa na ubunifu wa bidhaa NMB

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAGUZI wa ndani kutoka nchi mbalimbali Afrika wamevutiwa na ubunifu wa bidhaa bora wa Benki ya NMB pamoja na uwekezaji wenye tija.

Akizungumza wakati wa Mkutano wa Wakaguzi wa Ndani wa Afrika (AFIIA 2024) uliofika tamati jana, Meneja wa tawi la NMB Clock Tower Arusha, Praygod Mphuru, alisema moja ya vitu vinavyowavutia wajumbe wanaowatembelea ni bidhaa ya NMB Pesa Akaunti kutokana na hasa urahisi na wepesi wa kuifungua.

Alisema NMB inatumia huduma hiyo, ambayo ni moja ya mikakati ya kufungua akaunti mpya za wateja ili kutekeleza ajenda yake ya kuwajumuisha Watanzania zaidi kifedha na kupeleka huduma vijijini.

"Tunautumia pia mkutano huu kwa ukubwa wake kama fursa ya kuonyesha umahili wetu wa kutoa huduma bora, ubunifu mkubwa wa bidhaa na jinsi tunavyowekeza vilivyo katika teknolojia mpya za kisasa," alisema Mphuru.

Alisema NMB pia inatoa elimu kuhusu huduma yake ya benki bima na bidhaa zake nyingi ambayo wajumbe wa AFIIA 2024 wameisifia kwa uharaka wake wa kuchakata fidia za wateja, vifurushi lukuki shindani ilivyonavyo na wepesi wa kuzilipia kinga zinazokatwa.

Alisema bidhaa nyingine kubwa kwenye banda la NMB zilizokuwepo ni ile ya nyumba ambayo kupitia kwake mteja anaweza kukopa hadi Sh. bilioni moja na kutumia nyumba anayomiliki kupata mkopo.

Alisema: "Wajumbe pia wamepata fursa ya kuyajua maeneo mengine ya huduma na bidhaa zetu mahsusi kwa kada mbalimbali za wateja ambazo ni pamoja na masuluhisho ya malipo, ufadhili wa biashara na mambo ya fedha za kigeni".

# Dk. Mwinyi aeleza umuhimu wa fani ya uwalimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema fani muhimu duniani ni ya uwalimu kwa sababu nchi haiwezi kupata wataalamu pasipo kuwa na walimu.

Aliyasema hayo jana visiwani Zanzibar wakati wa ufunguzi wa Shule ya Msingi ya Hamid Ameir iliyopo eneo la Donge, Mkoa wa Kaskazini Unguja ikiwa ni shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Alisema licha ya umuhimu wa walimu, lakini jambo la kusikitisha ni kwamba bado maslahi ya walimu ni duni ikilinganishwa na wataalamu wengine.

Alisema duniani nchi zilizopiga hatua katika elimu ni Norway kwa sababu hakuna fani wanazozipa kipaumbele zaidi kuliko uwalimu.

Dk. Mwinyi alisema lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuboresha mazingira ya elimu kwa kuweka sawa mazingira wezeshi ya sekta hiyo pamoja na kuimarisha maslahi yao.

Pia, aliahidi kuongeza uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya elimu kwa kuipa kipaumbele bajeti ijayo ya sekta hiyo, ili kuimarisha mazingira bora kutoka ngazi ya maandalizi, msingi hadi sekondari.

Alisema hatua hiyo inatarajiwa kuzaa matunda bora ya matokeo mazuri kwenye kuongeza kasi ya ufaulu kwa wanafunzi.

Pia, aliiagiza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuendeleza fursa za kuajiri walimu wengi zaidi wa fani zote ili kuondosha changamoto ya uhaba wa walimu Zanzibar.

Akizungumzia kuhusu miaka 60 ya Muungano, Dk. Mwinyi alisifu hatua za waasisi wa Muungano huo na wote waliojitolea kuutunza na kuuenzi.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdul Gulam Hussein alisifu jitihada za Dk. Mwinyi kwa uwekezaji mkubwa aliowekeza katika wizara hiyo.

Alisema wizara hiyo tayari imekamilisha ujenzi wa madarasa ya ghorofa 20 ndani ya kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Dk. Mwinyi na kuahidi kumalizia ujenzi wa skuli za ghorofa kwa majimbo yote ya Unguja na Pemba.

Aidha, alieleza Wizara ya Elimu na Mafuzo ya Amali tayari imeingiza makontena 60 ya vifaa vya skuli mpya zikiwemo meza, komputa, projekta, mashine za urudufishaji, vitanda kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Waziri wa Ujenzi na Mawasiliano, Dk. Khalid Salum Muhamed alimshukuru Dk. Mwinyi kwa kufanikiwa kupeleka miradi mingi jimboni kwake ikiwemo ujezi wa Soko la Donge Mtambile, Daraja la Donge Chechele.

Pia, alimpongeza kwa kuboresha barabara za vijijini pamoja na kuondosha msongamano wa wanafunzi kwa ujenzi wa shule za kisasa za ghorofa.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Rashid Hadid Rashid alimpongeza Dk. Mwinyi kwa kuinua sekta ya elimu Zanzibar.

Katibu wa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Idara ya Itikadi Uenezi na Mafunzo Zanzibar, Khamis Mbeto Khamis alisema, ilani ya chama hicho ya mwaka 2020 - 2025 ndio mkataba baina ya Serikali na wananchi.



Mwakilishi kutoka Chuo cha Utamaduni wa Urusi, Rifat Pateev (katikati), akizungumza na Katibu Mtendaji Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA), Dk. Mwanahija Ali Juma (kulia), alipotembelea Ofisi za Baraza hilo, Mwanakwerekwe Wilaya ya Magharibi B jana, kwa lengo la kuimarisha ushirikiano. **PICHA: MAELEZO**

# BAKIZA yapokea vitabu vya Kiswahili kutoka Urusi

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) limepokea vitabu vya Kiswahili vilivyochapishwa na Chuo cha Utamaduni Urusi ili kuikuza na kuiendeleza lugha hiyo.

Akipokea vitabu hivyo, Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Dk. Mwanahija Ali Juma alisema vitabu hivyo vitasaidia kuimarisha lugha hiyo sambamba na kujenga ushirikiano kati ya Urusi na Zanzibar.

Aidha aliutaka ujumbe kutoka Chuo cha Utamaduni Urusi kuendeleza ushirikiano uliopo kati yao ili kukieneza Kiswahili duniani. "Sisi kama baraza tuna jukumu la kuwaendeleza waandishi wachanga na kufanya mashindano ya uwandishi wa tungo mbalimbali kwa waandishi wakubwa na wadogo ili tuhakikishe lugha yetu inautmika kwa usahihi na ufasaha" alisema Dk. Mwanahija.

Alisema katika kuhakikisha lugha hiyo inafika mbali zaidi Baraza la Kiswahili Zanzibar limechapisha kamusi na vitabu mbalimbali pamoja na kufanya mashindano ya uandishi wa makala kwa waandishi wachanga na wanafunzi ili kuiendeleza lugha hiyo.

Dk. Mwanahija alisema kuwa baraza hilo ni taasisi iliyoanzishwa chini ya kifungu namba nne kwa lengo la kusimamia Kiswahili na kuhakikisha kinaenda mbele na kutumika katika mawasiliano duniani.


Mwakilishi wa chuo hicho, Rifat Pateev, alisema Urusi ni ya kwanza kuchapisha vitabu vya Kiswahili ikiwemo kitabu cha Shaaban Robert na Shafi Adam Shafi na hivi karibuni wameanza kuitumia lugha hiyo shuleni.

Aliongeza kuwa kwa sasa wapo Zanzibar kwa ajili ya kujifunza zaidi lugha ya Kiswahili pamoja na kujenga uhusiano na Wazanzibar ili kuiendeleza lugha hiyo.

Miongoni mwa vitabu vilivyopokelewa ni pamoja na kitabu cha ndege wa moto, bila ya mahari, tembo, sudi ya mwanadamu na koti la karani ambavyo vyote vimechapishwa kwa lugha ya Kiswahili na vinatumika nchini kwao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**REHENI REHANI SAID** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0187-0037** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **AN-NOOR ISLAMIC BOYS SEMINARY** mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MOR/IFA/8922/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IVONA AGUSTINO KALENZI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye majina **BEATUS ALKADO MALEMA** namba za usajili *T 914 DPT* aina ya **LANDCRUISER,** Chassis No. **JTECB09J603018712,** Engine No. **1HZ0459745.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

TAARIFA YA POLISI:

**PHQ/DOD/DOD/13333/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAZAQ JUMA MMBAGA**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usaliji **T 198 BGW** aina ya SCANIA yenye Chassis namba **04361528.** Yeyote atayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:

**PHQ/DAR/ILA/63387/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GOD ENOCK VAHAYE**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 365 AAQ.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi:

**PHQ/IRE/IRI/4750/2024**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO CAUSE No 6936 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late RODA DANIEL KIJO**

**And**

**In the Matter of Application for Letters of Administration by FESTO DANIEL KIJO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN NO. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on before the 21 day of MAY 2024. 8:00am

Dated at DAR ES SALAAM this 9TH day of APRIL 2024.

Resident Magistrate

---

**FORM NO 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO CAUSE No 6808 of 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late DANIEL MANASE KIJO**

**And**

**In the Matter of Application for Letters of Administration by FESTO DANIEL KIJO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN NO. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on before the 03rd day of MAY 2024.
Dated at DAR ES SALAAM this 12TH day of APRIL 2024

Senior Resident Magistrate

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO BOMA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...20/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: RAJABU ABDUL KIHARA wa SULTAN AREA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA ALLY ABDUL KIHARA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 23 Mwezi 04 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 05 mwezi 04 mwaka 2024

HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha MAKOLE Mkoa DODOMA**

**Shauri la MIRATHI Na 47/2012**

**Jina la MWOMBAJI: ROSEMARY MAZENGO**

**Jina la MAREHEMU: PETER MAZENGO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za utaratibu Madai Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa PAULO PETER MAZENGO**
**KISASA**
**SIMU NO 0625664009**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai)**

**WITO WA MAHAKAMA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 29 Mwezi 4 Mwaka 2024 Saa 08:30 asubuhi/Mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku yakusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikathibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 18 Mwezi 4 Mwaka 2024.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MAKOLE - DODOMA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**

**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...10/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: SAIDA AHMAD ATHUMANI WA M/SONGO - MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA AHMAD ATHUMANI NYANZA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 22 Mwezi 04 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 12 mwezi 04 mwaka 2024

HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...11/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: OMARY ISMAIL MAGOMBA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA AZIZA OMARY ISMAIL**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 23 Mwezi 4 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 16 mwezi 04 mwaka 2024

HAKIMU

---

## TANGAZO LA NOTISI WADAIWA

**TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICE LIMITED,** Inatangaza notisi kwa wadaiwa waliokopa mikopo na kushindwa kulipa madeni yao kama ifuatavyo:-

PAMELA. E. SAIMON wa Dar Es Salaam notisi ya siku kumi na nne **(Siku 14)** kutakiwa kulipa deni lako.

LYDIA JOSEPHAT MAGESSA wa Dar Es Salaam notisi ya siku thelathini **(Siku 30)** kutakiwa kulipa deni lako.

EMMANUEL PANDA NGHWANI wa Mwanza Notisi ya siku sitini **(Siku 60)** kutakiwa kulipa deni lako.

Mnatakiwa kulipa madeni yenu ya mikopo mnayodaiwa na Tujijenge ndani ya muda husika ulioainishwa mbele ya jina lako.
Hii ni baada ya mkopo kushindwa kulipwa kulingana na masharti na makubaliano ya mkataba.

Notisi hii itatumika kuanzia tarehe ya Tangazo hili gazetini. Hatua zaidi za Kisheria zitachukuliwa dhidi yako endapo kama utashindwa kulipa deni la mkopo ndani ya muda ulioainishwa/kutangazwa.

Ikiwa ni pamoja na kufuata taratibu nyingine za kisheria au kuruhusu dalali kuuza mali zilizotumika kudhamini mkopo uliochukuliwa.

**Kwa Mawasiliano piga:**
**+255 222774742-3/0677088251/0718068335**
**Au Email: tujijengetanzania@tujijenge.or.tz**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MOROGORO**

**SHAURI LA MIRATHI NO......7018/2024**

**MWOMBAJI: ............MARIA THOMAS ANTHONY**

**MAREHEMU:......THOMAS ANTHONY MALAMLA**

**TANGAZO**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Mwombaji hapo juu.

Pingamizi lolote kuhusu ombi hili liwe limeandikwa hapa mahakamani mnano au kabla ya tarehe 20/05/2024.

Imetolewa leo tarehe 05/04/2024

HAKIMU MKAZI
MOROGORO
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
MOROGORO


KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie, 0782253676*

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail:**
**advertise@guardian.co.tz,**
**website:**
**www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# TAKUKURU yabaini kasoro miradi bil.9/-

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma, imebaini upungufu katika miradi 10 yenye thamani ya Sh. bilioni 9.9 inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali mkoani hapa ambayo wahusika wamechukuliwa hatua za kisheria.

Aidha, TAKUKURU imebaini sekta ya elimu inaongoza kwa kulalamikiwa na masuala ya rushwa kwa asilimia 14, ikifuatiwa na Ofisi ya Rais tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa asilimia 13.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, John Joseph, alisema upungufu waliobaini ni pamoja na utumiaji wa nondo zilizo chini ya kiwango, matumizi ya mbao hafifu katika utengenezaji milango na ujenzi kutoendana na thamani halisi ya fedha.

Kasoro zingine, alisema ni pamoja na baadhi ya wazabuni kulipwa fedha kabla hawajawasilisha vifaa, suala linalochangia kuwasilisha vifaa pungufu ambavyo havijafanyiwa ukaguzi.

"Tunaendelea kufuatilia miradi hiyo tunahitaji kuona inatekelezwa kwa thamani halisi uliotolewa na serikali kwa wazabuni,"alisema Joseph.

Pia alisema upungufu huo umesababisha kufunguliwa majalada ya uchunguzi katika baadhi ya miradi inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali, huku akibainisha miradi 52 inayotekelezwa vizuri ambayo ni ya elimu, ujenzi, afya, maji na utawala.

Kuhusu asilimia za viashiria vya vitendo vya rushwa na asilimia kwenye mabano, alisema ardhi inashika nafasi ya tatu kwa kuwa na asilimia 12,ikifuatiwa na maji (9), fedha (nane), kilimo (saba) huku taasisi nyingine zikiwa na asilimia moja.

Pia alisema wanafanyia kazi ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) na kuitumia kufuatilia vitendo vya rushwa katika maeneo mbalimbali.

Aidha, alisema TAKUKURU itaendelea kutoa elimu ya kupinga rushwa mahali pa kazi, shuleni na vyuoni.

# Ghorofa laporomoka, laua na kujeruhi watu wanane

**Na Romana Mallya**

FUNDI ujenzi aliyefahamika kwa jina la Omary, maarufu kama Mwarabu, amefariki dunia na wenzake wanane kujeruhiwa baada ya jengo la ghorofa mbili lililokuwa likijengwa Kata ya Tungi, Mtaa wa Magogoni, Kigamboni mkoani Dar es Salaam, kuporomoka.

Ofisa Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Kigamboni, Mkaguzi Innocent Ingbertus, alisema tukio hilo lilitokea juzi mchana na kumtaja mmiliki wake kuwa ni Irfan Hassan na mhandisi mjenzi ni Shabani Kapinga, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya ujenzi ya Azhar.

"Katika tukio hili amekufa mtu mmoja na majeruhi wanane walipelekwa Kituo cha Afya Kigamboni. Chanzo cha kuporomoka kwa ghorofa hili ni ujenzi holela bila kufuata taratibu za ujenzi," alisema.

Ingbertus alisema wakati ghorofa hilo likiporomoka, baadhi ya mafundi walikuwa sehemu ya juu na wengine chini.

"Siku hiyo (juzi) waliingia mafundi 16 kwa ajili ya ujenzi na katika tukio hili waliojeruhiwa ni wanane na mmoja amefariki dunia. Katika taratibu za ujenzi lazima wapate kibali kutoka manispaa, lakini sheria na kanuni ya ukaguzi ya mwaka 2015 lazima wawasiliane na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

"Kwa hiyo kuna taratibu hazikufuatwa, kwa hiyo tunaweza kusema ni ujenzi holela haukufuata taratibu. Mhusika wa jengo alifikishwa polisi jana (juzi) kwa ajili ya mahojiano," alisema.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, alisema Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na mamlaka zingine za kiuchunguzi zenye uhusiano na majengo, wanaendelea kuchunguza kujua kwa kina nini kilisababisha ajali hiyo na kwamba, watu mbalimbali watahojiwa.

Desemba 18, 2022 watu watano walifariki dunia na wengine tisa kujeruhiwa baada ya kuangukiwa na jengo la ghorofa mbili, katika Kijiji cha Sembeti, Marangu, Moshi mkoani Kilimanjaro, wakati mafundi na vibarua wakiendelea kumimina zege.

**TAMKO LA SERIKALI**

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, katika taarifa yake jana, alizielekeza bodi za usajili wa wahandisi (ERB), usajili wa makandarasi (CRB) na ya wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi (AQRB) kufika mara moja eneo la tukio na kushirikiana na timu za wataalam kutoka mamlaka zingine za serikali kupata sababu kuanguka jengo hilo.

Bashungwa pia aliwataka kuchukua hatua stahiki kwa wale wote waliokiuka sheria za kitaalamu katika ujenzi na usimamizi wa jengo hilo.

Waziri pia alizitaka bodi hizo kuhakikisha wanaendelea kusimamia miradi ya ujenzi ikiwamo barabara, madaraja na majengo na kuhakikisha wajenzi na wasimamizi wa miradi wanafanya kazi kwa kuzingatia miiko na maadili ya taaluma zao.

Aidha, alitoa pole kwa majeruhi na familia iliyopoteza mpendwa wao na kutoa wito kwa makandarasi, wahandisi wa majengo kutumia wataalam waliosajiliwa na CRB,ERB na AQRB ili kuepuka kutokea madhara yanayoweza kusababisha kifo au kujeruhi.



Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa (kushoto), akizungumza na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, Happiness Laizer wakati wa Mkutano wa 10 wa Shirikisho la Taasisi za Wakaguzi wa Ndani Afrika (AFIIA), jijini Arusha jana. Katikati ni Meneja Mahusiano Huduma za Serikali wa NMB Kanda ya Kaskazini, Peter Masawe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge ataka kupitiwa upya leseni za kubeti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Mlalo (CCM), Abdallah Shangazi, amesema vijana wa kiume ni waathirika wa michezo ya kubashiri (kubet) hali inayosababisha ukatili wa kingono, kiuchumi na kujidhuru mwili.

Akiuliza maswali bungeni jana, alisema hali hiyo inasababisha tatizo la afya ya akili na kuhoji kama serikali ipo tayari kupitia utoaji leseni wa kampuni za kubashiri hasa za bonanza.

"Kwa kuwa michezo ya kubashiri mitandaoni inafanya vizuri na ipo chini ya Wizara ya Fedha, je serikali ipo tayari kuihamisha bodi ya michezo kutoka Wizara ya Fedha na kupeleka Wizara ya Michezo," alisema.

Aidha, alihoji serikali inatambua athari hasi kwa jamii ya Watanzania zinazotokana na ongezeko kubwa la michezo ya kubahatisha.

Akijibu maswali hayo, Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, alisema pamoja na faida za kiuchumi na kijamii zinazotokana na michezo ya kubahatisha, serikali inatambua athari zake katika jamii endapo haitaendeshwa kwa weledi.

Alisema miongoni mwa athari hasi zinazoweza kujitokeza katika jamii ni uraibu na kugeuza michezo ya kubahatisha kuwa mbadala wa ajira, ushiriki wa watoto katika michezo ya kubahatisha na michezo haramu ambayo haina usajili wa mamlaka ya udhibiti.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 7(2)(i) cha Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41, mamlaka ya udhibiti ina jukumu la kuhakikisha kuwa jamii inalindwa ipasavyo dhidi ya athari hasi za michezo ya kubahatisha.

Katika kutekeleza jukumu hilo, alisema Bodi ya Michezo ya kubahatisha inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuzuia na kudhibiti athari hasi zitokanazo na michezo ya kubahatisha.

Alisema mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha udhibiti na uratibu wa sekta kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na matumizi ya mifumo ya Tehama.

Pia, kutoa elimu kwa jamii kuhusu athari za michezo ya kubahatisha, kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mifumo ya usimamizi wa michezo ya kubahatisha na kufanya kazi ya udhibiti kwa kushirikisha wadau na mamlaka nyingine kama Jeshi la Polisi, TCRA na TRA.

# UHAMIAJI FC, BLACK SAILOR HAPATOSHI KOMBE LA ZFF

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Uhamiaji 'Wanajeshi wa Mipakani' wamesema wanahitaji kupata ushindi katika mechi ya hatua ya 16 bora ya mashindano ya Kombe la ZFF (FA Cup) dhidi ya Black Sailor (pichani) itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Mau B ili wafikie malengo yao.

Kauli hiyo ya Uhamiaji imetolewa baada ya kupoteza matumaini ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.

Kocha Mkuu wa Uhamiaji, Abdul Saleh Mohammed, akizungumza na gazeti hili jana alisema amewaandaa vyema wachezaji wake ili wasonge mbele ingawa anakiri michuano hiyo ni migumu.



**Kocha huyo alisema wapinzani wao wana kikosi imara huku wakiwa na msimu mzuri katika Ligi Daraja la Kwanza.**

Aliongeza licha ya kukabiliwa na mechi za Ligi Kuu Zanzibar, kwa sasa nguvu na akili zao wamezielekeza zaidi katika mashindano ya ZFF na anaamini uwezo wa kushinda wanao.

"Tunashuka kucheza na Black Sailor ambayo si timu ya kubeza, nimekiandaa vyema kikosi changu ili tushinde na hatimaye kusonga mbele hatua inayofuata," alisema kocha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Black Sailor, Juma Awadh Khatib, alisema yupo tayari kupambana kusaka ushindi katika mchezo huo muhimu.

Khatib alisema amekiandaa vizuri kikosi chake na wataingia uwanjani wakiwaheshimu wapinzani wao kutokana na wachezaji wao kuwa na uzoefu. Aliongeza wanaijua vyema Uhamiaji kwa sababu wameshakutana nao mara nyingi lakini pamoja na yote dakika 90 za mechi hiyo ndio zitaamua nani atakayesonga hatua inayofuata.

Mechi nyingine ya mashindano hayo itakuwa ni kati ya Mlandege dhidi ya Inter Zanzibar, itachezwa kwenye Uwanja wa Mao Zedong A.

Bingwa wa mashindano hayo atapata tiketi ya kuiwakilisha Zanzibar katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho ambayo huandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

# *Mashujaa yachekelea sare*

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Mashujaa FC wameipongeza timu yao baada ya kutoka sare ya bila kufungana na Azam katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi.

Mwenyekiti wa timu hiyo, Meja Abdul Tika, aliliambia gazeti hili jana wachezaji wao walionyesha kiwango cha kuu katika mchezo huo ambao ulikuwa na upinzani mkubwa.

Tika alisema siri kubwa ya kugawana pointi ilitokana na wachezaji wao kuwaheshimu wapinzani na kujitoa katika dakika zote 90 za mchezo huo.

"Ninawapongeza wachezaji wetu kutokana na juhudi walizozionyesha katika mchezo huo na kufanikiwa kutoka sare na timu ambayo ina wachezaji wengi wazoefu na wakimataifa," alisema Tika.

Alisema wameshaondoka Dar es Salaam na kuelekea Mwanza kwa ajili ya kujiandaa na mchezo dhidi ya Yanga utakaopigwa Mei 8, mwaka huu.

Aliongeza malengo yao ni kuendelea kufanya vizuri na kujiimarisha katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na kusonga mbele kwenye michuano ya Kombe la FA ambayo watachuana katika hatua ya robo fainali.




Kiungo wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto' (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa Mashujaa katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi usiku. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: MTANDAO**

## Tabora United FC hali tete Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kubadilisha kocha, bado hali ni mbaya kwa Tabora United baada ya kukubali kichapo cha mabao 3-0 dhidi ya Kagera Sugara ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani, Tabora.

Baada ya kufanya vibaya, klabu hiyo ilimwondoa Kocha, Goran Copunovic na kumleta Mfaransa Denis Goavec, ambaye mpaka sasa bado hajashinda mechi yoyote ya Ligi Kuu.

Tangu awasili katika timu hiyo, Goavec ameiongoza Tabora United katika mechi tatu, akishinda mchezo wa Kombe la FA dhidi ya Singida Big Stars lakini iliporudi nyumbani ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya JKT Tanzania.

Mabao ya Kagera Sugar katika mechi ya juzi yaliwekwa wavuni na Mubarack Amza, dakika ya 24, Obrey Chirwa (dk ya 48) na Mbaraka Yusuph akifunga goli la tatu dakika ya 72.

Timu hiyo zamani ikijulikana kwa jina la Kitayosce ilipanda daraja msimu ipo katika hatari nafasi mbaya kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikishika nafasi ya 15 baada ya kujikusanyia pointi 22, imecheza mechi 23, ikibakisha saba tu kumaliza msimu.

## ZFF na mipango kuwanoa vijana

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), limesema litaandaa mkakati maalum wa kuwaendeleza vijana ambao wamefanya vizuri katika programu ya kusaka vipaji iliyosimamiwa na wakufunzi kutoka Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), imeelezwa.

Nyota 49 wamefaulu katika programu hiyo iliyoshirikisha awali wachezaji 500 na kati ya waliofaulu kundi la kwanza lenye vijana 27 wana umri chini ya miaka 17 (U-17) na waliobakia ni U-15.

Akizungumza na gazeti hili, Mkurugenzi wa Ufundi wa ZFF, Masoud Atai, alisema mpango huo utakwenda sambamba na maagizo yaliyotolewa na wakufunzi hao ili kuhakikisha wanafanikiwa katika kuwaendeleza vijana hao.

Atai alisema mkakati wa kwanza wa ZFF ni kuchagua makocha wenye sifa na vigezo vyote ili kuwaongoza vijana hao kisoka kama inavyotakiwa.

"Wataalam waliokuja wametupa moyo kama Zanzibar vipaji vipo tena sana, changamoto iliyopo ni kuwaendeleza hawa vijana kiutaalam zaidi, hivyo mapema tutayafanyia kazi maagizo yao ili kuhakikisha tunafikia malengo,"Atai alisema.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### OLMO ATAKIWA BARCA

BARCELONA na Manchester City zimefanya mazungumzo na wawakilishi wa kiungo wa kati wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Hispania, Dani Olmo, mwenye umri wa miaka 25, wiki iliyopita. ***(Mundo Deportivo)***

#### DYBALA AREJEA SOKONI

CHELSEA na Barcelona ni miongoni mwa klabu kadhaa za Ulaya zinazofikiria kumnunua mshambuliaji wa AS Roma, mwenye umri wa miaka 30 kutoka Argentina, Paulo Dybala. ***(Rudy Galetti)***

#### MARQUEZ KUMRITHI XAVI

MLINZI wa zamani wa Mexico, Rafa Marquez, ni mmoja wa wanaowania kurithi mikoba ya Xavi wakati Mhispania huyo atakapojiuzulu kama kocha wa Barcelona mwishoni mwa msimu huu. ***(ESPN)***

#### BRANTHWAITE AGEUKA LULU

KLABU za Bayern Munich na Tottenham Hotspur zimeungana na Manchester United katika kufikiria kumnunua beki wa Everton mwenye umri wa miaka 21, Jarrad Branthwaite. ***(TeamTalks)***

#### GUEYE ATAJWA SAUDIA

KLABU za Ligi Kuu Hispania (Saudi Pro League), zinavutiwa na kiungo wa kati wa Senegal, Idrissa Gana Gueye, mwenye umri wa miaka 34, ambaye huenda asipewe ofa mpya na Everton mkataba wake utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu. ***(Football Insider)***

#### DIOMANDE ANUKIA LIVERPOOL

KLABU za Newcastle United na Liverpool zimeingia katika kinyang'anyiro cha kumsajili beki wa Sporting Lisbon mwenye umri wa miaka 20 kutoka Ivory Coast, Ousmane Diomande, ambaye pia anasakwa na Chelsea. ***(Football Transfers)***

#### ZENON ANUKIA NEWCASTLE

NEWCASTLE United imetuma maskauti kuwatazama kiungo wa Boca Juniors raia wa Argentina, Kevin Zenon, mwenye umri wa miaka 23 na mlinzi wa Argentina, Nicolas Valentini (23). ***(HITC)***

#### DYCHE KUBAKIA EVERTON

KAZI ya Sean Dyche kama kocha wa Everton haiko hatarini licha ya matokeo mabaya ya klabu hiyo. ***(News)***

#### THAMANI MURILLO YATAJWA

KLABU ya Nottingham Forest inataka zaidi ya pauni milioni 20 ili kumuuza beki wa kati wa Brazil, Murillo mwenye umri wa miaka 21, huku Liverpool, Chelsea, Manchester United na Paris St-Germain pia zikimnyatia. ***(Football Insider)***

#### UTD KUMUUZA GREENWOOD

KLABU ya Manchester United inaweza kumuuza Mason Greenwood kama sehemu ya mpango wa kumsajili beki wa Brazil, Gleison Bremer, mwenye umri wa miaka 27, kutoka Juventus. ***(Gazzetta dello Sport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA U



# GUARDIOLA: TULIPAMBANA, TULIONYESHA KIWANGO BORA

**MADRID,** Hispania

**●●● Kocha huyo asema hawakuwa na bahati, aipongeza Madrid kwa...**

PEP Guardiola amesema "sitawahukumu" Real Madrid kwa aina yao ya uchezaji baada ya kuwaondoa Manchester City katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa penalti.

**Manchester City walitawala mchezo baada ya bao la mapema la Rodrygo, lakini walisawazisha kupitia kwa Kevin De Bruyne.**

"Sihukumu," alisema Guardiola, alipoulizwa kama alishangazwa na mfumo wa ulinzi wa Real Madrid.

"Tumegundua wapinzani wa aina hiyo huko nyuma, timu zingine ziko wazi zaidi, zingine zinacheza kwa kukamia sana. Wanajua ni uwanja mgumu kufika na wamejaribu. Tuliwasukuma sana, haswa kipindi cha pili.

"Tulikuwa ukingoni katika eneo la hatari na tukapiga mashuti mengi kutoka nje ya eneo hilo, lakini hatukufanikisha hilo. Tulifanya kila tuliloweza lakini mwisho hatukufanikiwa."

City walipata nafasi katika muda wa kawaida, lakini walishuhudia mpira wa kichwa wa Erling Haaland wa kipindi cha kwanza ukigonga mwamba wa goli na De Bruyne akiruka juu kutoka ndani ya eneo la hatari na matokeo kuwa 1-1.

"Ningependelea kushinda, lakini pongezi kwa Real Madrid," aliongeza Guardiola. "Tulifanya kila kitu, kwa hivyo sijutii chochote tulichofanya.

"Tulicheza kwa kiwango cha kipekee, lakini kwa bahati mbaya hatukushinda kwa hivyo ndivyo ilivyo. Nalazimika kusema asante kwa wachezaji hawa kutoka ndani ya moyo wangu kwa jinsi walivyocheza. Lakini mpira ni kushinda na hatukufanya hivyo kutosha bado tulikuwa wa kipekee.

"Wakati mwingine unaweza kushinda kwa penalti na wakati mwingine huwezi. Lakini katika mchezo hatukubadilisha nafasi ambazo tulipata."

Baada ya dakika 120 za soka zenye kuchosha na kukatishwa tamaa kwa kushindwa kwenye mikwaju ya penalti, Guardiola anakabiliwa na kibarua kigumu kuwainua wachezaji wake kwa ajili ya nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Chelsea utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Wembley.

# TUCHEL AWAJIA JUU WAKOSOAJI WAKE




**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel, aliwajia juu wakosoaji wake baada ya kuiongoza timu hiyo ya Bundesliga kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Arsenal hapo juzi.

Bayern Munich hawatashinda taji lolote la ndani msimu huu baada ya utawala wao wa miaka 11 kama mabingwa wa Bundesliga kukomeshwa na Bayer Leverkusen na mwenendo wao mbaya ukasababisha wakubwa wa klabu hiyo kuamua kuachana na Tuchel mwishoni mwa msimu huu.

Alipoulizwa baada ya ushindi wa Jumatano kwenye Uwanja wa Allianz Arena kama alijisikia kuridhika kutokana na jinsi msimu wake ulivyokuwa na Bayern, Tuchel alisema: "Lakini ukosoaji ulitoka wapi. Kutoka kwenu, vyombo vya habari, na sasa mnaniuliza kama ninahisi kuridhika.?"

"Ndivyo ilivyo. Nimejitoa tangu siku ya kwanza na nitatoa yote hadi siku ya mwisho," alisema.

Bavaria hao walishinda kwa bao la kichwa la Joshua Kimmich dakika ya 63 lililowapa ushindi wa jumla wa 3-2 katika mechi zote mbili, huku rais wa Bayern, Herbert Hainer akiusifu ufundishaji wa Tuchel kama 'ufundi bora wa kimbinu.'

Matokeo ya Jumatano yanamaanisha Tuchel amekuwa Mjerumani wa kwanza kuongoza klabu kutoka nchi tatu tofauti hadi angalau nusu fainali ya shindano hilo baada ya kushinda taji na Chelsea mnamo 2021 na kuiongoza Paris Saint-Germain hadi fainali mnamo 2020.

"Nusu fainali ni hatua kubwa. Nne za mwisho, hiyo ilikuwa ya kufurahisha. Furaha kubwa na ahueni kubwa," alisema Tuchel akiwaambia waandishi wa habari.

"Hizi ni nyakati maalum. Tulishinda moja ya klabu za juu za Ligi Kuu. Itabidi tuone ushindi huu utafanya nini kwa klabu. Msimu bado haujaisha."

# 'Wirtz hauzwi kwa bei rahisi'

**LEVERKUSEN,** Ujerumani

KLABU ya Bayer Leverkusen imeapa kutomuuza, Florian Wirtz, kwa bei ya chini na inataka kumfanya awe mchezaji wa nne ghali zaidi wa muda wote.

Akiwa amefunga mabao 35 na kutoa pasi za magoli kadhaa katika mechi 41 alizocheza kwenye michuano yote, Wirtz amekuwa msingi wa mafanikio ya Leverkusen msimu huu, ikiwa ni pamoja na kunyakua taji la kwanza kabisa la Bundesliga mwishoni mwa juma baada ya miaka 120.

Nyota wengi wa timu hiyo wanavutia watu kutoka kote Ulaya, huku Wirtz akiwa ndiye kito katika taji hilo.

Manchester City kwa muda mrefu wamekuwa wakimtaka mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 20 lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Liverpool na Bayern Munich.

Pia Real Madrid wamekuwa wakihusishwa katika siku za hivi karibuni, huku kukiwa na tetesi zinazoendelea kuhusu Barcelona, Arsenal, Chelsea na Manchester United.

Lakini Leverkusen wamechora mstari thabiti kwenye mchanga juu ya uthamini.

"Hakuna mtu asiyeweza kuuzwa, lakini Wirtz hataondoka kwa chini ya euro milioni 150," alisema mtendaji mkuu wa Klabu hiyo, Fernando Carro akiiambia Radio Marca wiki hii.

Kiasi hicho, ambacho ni sawa na pauni milioni 128 kitamaanisha Neymar, Kylian Mbappe na Philippe Coutinho pekee ndio wamewahi kugharimu bei kubwa zaidi.

Wakizungumza Desemba, babake Wirtz na wakala walipendekeza mpango wa haraka wa mchezaji huyo ni kubaki na Leverkusen, ambapo ana mkataba hadi 2027.




# Kipigo hakijaharibu msimu wetu - Arteta



**MUNICH,** Ujerumani

MIKEL Arteta amesema wachezaji wake wa Arsenal wanahisi uchungu wa kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Bayern Munich, lakini akasisitiza haitaharibu msimu wao.

Washikabunduki hao walitupwa nje katika hatua ya robo fainali kwa bao la Joshua Kimmich katika mechi ya mkondo wa pili na kuwapa Bayern ushindi wa jumla wa 3-2.

Arsenal wanakabiliwa na mabadiliko ya haraka kwa safari dhidi ya Wolves hapo kesho huku wakilenga kuwafukuza vinara wa Ligi Kuu England Manchester City zikiwa zimesalia mechi sita.

Arteta alisema: "Maumivu yapo, lakini ninaweza kukuhakikishia kufikia kesho tutakuwa tumezingatia kikamilifu mchezo dhidi ya Wolves na kila mtu ameinuliwa.

"Tunachotakiwa kucheza bado ni kizuri, nilisema kabla ya muda wa kuwa karibu na hawa wachezaji ni rahisi kuwa nyuma yao na kuwasifu wachezaji na kuzungumza mambo mazuri tunaposhinda 10 mfululizo na sare moja, sasa ni wako nyuma yao na kuwa karibu nao."

"Hatujacheza shindano hili kwa miaka saba na hatujakaa katika hatua hii kwa miaka 14," alisema Arteta.

"Kuna sababu yake. Tunataka kufanya kila kitu kwa kasi mbele, haraka sana katika msimu mmoja. Nadhani tuna uwezo na ubora wa kuingia nusu fainali."

# Yanga yamalizana na Mzize 'kibabe'

INATOKA UKURASA 24

miwili na hivyo kumaliza ndoto za matajiri hao wa Chamazi kupata huduma yake kwa ajili ya msimu ujao.

Azam ambayo iliweka mezani ofa ya Sh. milioni 400 ili kumnunua Mzize ambaye anatajwa pia kutakiwa na timu moja ya England pia inataka kumsajili kiungo mshambuliaji wa Simba, Mzambia Clatous Chama.

Hata hivyo katika barua ya Azam, hakuna mahali ilikoandika katika maombi ya kumsajili Mzize, kutakuwa na makubaliano ya kubadilishana na mshambuliaji wake nyota, Prince Dube, ambaye kwa sasa yuko katika mgogoro na timu hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari Msaidizi wa Azam FC, Hashim Ibwe (pichani), alikiri wamepeleka ofa katika klabu hizo mbili (Yanga na Simba), kwa ajili ya kuhitaji kuwapata nyota wanne ambao watakiongezea nguvu kikosi chao.

Ibwe alisema mbali na kuweka dau kubwa kwa Mzize, pia wameahidi watamlipa mshahara kubwa endapo dili ya kumnasa mshambuliaji huyo litafanikiwa.

"Hatuishii kwa Yanga pekee pia tutaenda kwa Simba, wiki ijayo kuanzia Jumatatu tunapeleka ofa nyingine kwenye moja ya hizi klabu tukihitaji huduma ya moja ya mchezaji wao," alisema Ibwe.

Ofisa huyo aliongeza mwaka huu wamedhamiria kufanya usajili 'mkubwa' kwa kuwanasa wachezaji 'muhimu' kutoka ndani ya klabu hizo mbili.

"Tumedhamiria na tuna mpango wa kusajili wachezaji wanne kutoka kwa Simba na Yanga, wachezaji hao ni pamoja na wazawa na wakigeni, tumejipanga kweli kweli," Ibwe alisema.

Aliongeza wameamua kufanya 'kweli' katika mchakato huo ili kuhakikisha msimu ujao wanakuwa na kikosi imara na kitakachowapata matokeo rafiki katika mashindano yote watakayoshiriki.



"Hatutaki masihara katika ofa hizo hakuna sehemu ambayo tunahitaji kubadilishana wachezaji bali, tumeweka ofa mezani," aliongeza Ibwe.

# VITA LIGI KUU WANAWAKE KUENDELEA VIWANJA VITANO

**Na Saada Akida**

RAUNDI ya 11 ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara itaendelea tena leo ambapo mabingwa watetezi, JKT Queens watakuwa nyumbani kuwakaribisha Geita Gold FC huku Simba Queens ikiwavaa wenyeji Baobab Queens kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma jijini, Dodoma.

Amani Queens watawakaribisha Yanga Princess katika dimba la Ilulu mkoani, Lindi huku Ceasiaa Queens ya Iringa bado wako nyumbani kucheza dhidi ya Fountain Gate Princess na Alliance Girls watawaalika Bunda Queens kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini, Mwanza.

**Kocha Msaidizi wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', alisema wamewasili salama Dodoma na wachezaji wake wapo tayari kwa ajili ya mchezo huo huku lengo lao kubwa ni kutafuta pointi tatu.**

Mgosi alisema ajenda yao ya kwanza katika mzunguko wa pili wameianza kwa mafanikio ambapo walipata ushindi wa bao 1-0 ugenini na sasa wanahitaji kutafuta alama tatu nyingine watakapoivaa Baobab Queens.

"Tangu msimu unaanza ninasema tunahitaji kurejesha heshima ya klabu, kufikia malengo hayo lazima tushinde mechi, hatuwadharau Baobab Queens licha ya kupitia changamoto nje ya uwanja, tutacheza kwa tahadhari kubwa," alisema Mgosi.

Kocha Mkuu wa JKT Queens, Esther Chabruma, alisema kutokana na maandalizi waliyofanya, anaimani kikosi chake kitaendelea kubakiza pointi tatu katika uwanja wao wa Meja Jenerali Isamuhyo.

Chabruma alisema mechi ya kwanza walifanikiwa kuvuna pointi tatu na sasa wanahitaji ushindi kwa ajili ya mipango yao ya kuhakikisha wanatetea taji la ubingwa walolishikilia.

"Bado hatujakata tamaa katika mbio za ubingwa, ligi inaendelea na tumejiandaa vizuri na mchezo wetu dhidi ya Geita Gold FC, kikubwa ni kuvuna pointi tatu," alisema Chabruma.

Kocha wa Fountain Gate Princess, Alex Alumirah, " Ni mechi ngumu,Ceasiaa Queens ni timu nzuri ukiangalia katika msimamo wako nafasi ya nne, sisi tupo ya tano, tunahitaji kupanda juu lazima tushinde hii mechi.

Nafurahi mechi ya kwanza hatukuruhusu bao na wala kufunga, tumefanyia kazi mapungufu yetu na sasa tuko tayari kwa mchezo huo wa ugenini," alisema Alumirah.



Kikosi cha mabingwa wapya wa Ligi ya Mabingwa wa Mikoa, Gunners FC ya jijini, Dodoma. **PICHA: TFF**

# Gunners bingwa Ligi ya Mikoa

**Na Adam Fungamwango**

WENYEJI Gunners wametwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Mikoa baada ya kuifunga Hausung FC ya Njombe bao 1-0 katika mechi ya fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma juzi.

Bao pekee katika mchezo huo lilifungwa na Fadhili Suleiman dakika ya 25, hata hivyo timu hizo mbili zilizocheza fainali zimepanda daraja na zitashiriki Ligi Daraja la Pili 'First League' msimu ujao.

Timu nyingine iliyofanikiwa kupanda daraja ni Moro Kids ambayo iliiadhibu Arusha City mabao 3-0 katika mechi ya awali kutafuta mshindi wa tatu.

Mabao ya washindi yalifungwa na Said Hamisi, aliyepachika mabao mawili dakika ya 38 na 90, na Mohamed Salehe aliyefunga goli dakika ya 59.

Mchezaji wa Gunners, Costa Mwihoneke, alipata tuzo mbili kwa kuwa mfungaji bora wa ligi hiyo, pamoja na mchezaji bora huku tuzo ya kipa bora ilikwenda kwa Mudhihir Jaffar wa Gunners na kocha wa timu hiyo, Juma Ikaba ambaye ni kiungo wa zamani wa CDA ya Dodoma, alichaguliwa kuwa kocha bora.

# Simba hatari vichwa, Yanga ndani ya boksi

INATOKA UKURASA 24

Simba inaonekana ina mabao mengi iliyofungwa mguu wa kulia, ikifanya hivyo mara 29 na kuizidi Yanga bao moja, lakini haina matumizi mazuri na mguu wa kushoto kwa wachezaji wake, wamefunga mabao sita tu wakati wenzao wana mabao 20.

Simba inaonekana ni hatari katika kutengeneza penalti, imefunga mabao saba ya mikwaju hiyo mpaka sasa, matano zaidi ya wapinzani wao, ikifunga mabao matano ya vichwa, ya kona matatu, huku ikipata mabao saba yaliyotokana na mipira ya krosi.


Yanga ambao ndio vinara wamecheza mechi 21 wakiwa na pointi 55 kibindoni wakati Simba yenye pointi 46 na iliyoko katika nafasi ya tatu kwenye msimamo imecheza michezo 20 ya ligi hiyo ya juu Tanzania Bara.

JKT Tanzania yenye pointi 22 sawa na Mashujaa FC pamoja na Tabora United, Mtibwa Sugar yenye pointi 17, ndio timu zilizoko mkiani katika msimamo wa ligi hiyo yenye timu 16.

# Michezo

Ijumaa Aprili 19, 2024

Nipashe


'Wirtz hauzwi kwa bei rahisi' UKURASA 22

KUELEKEA DABI




Chama

Mzize

# Simba hatari vichwa, Yanga ndani ya boksi

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Matokeo ya mechi ya kesho yatatoa 'picha' ya mbio za kuwania ubingwa...

WAKATI mechi ya watani wa jadi nchini inatarajiwa kuchezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, nguvu ya Simba ipo katika mipira ya kona na matumizi mazuri ya vichwa huku Yanga ambao ni wenyeji wa dabi hiyo inaonekana hatari zaidi ikiingia ndani ya eneo la hatari.

**Kwa mujibu wa takwimu za dawati la Nipashe zilizokusanywa kabla ya mchezo huo ambao huvuta hisia za mashabiki wa soka wa ndani na nje ya nchi, timu zote mbili zina maeneo ambayo ndiko inategemea kutumia kupata ushindi.**

Takwimu zinaonyesha Simba ina mabao matatu yaliyotokana na mipira ya kona, huku Yanga ikiwa haina hata bao moja lililotokana na njia hiyo.

Simba ina mabao matano yaliyofungwa kwa vichwa, wakati Yanga ikiwa imepachika magoli manne kwa njia hiyo, huku timu zote mbili zikifanana kwa kila moja kufunga kwa mipira ya faulo moja ya moja kwa moja, na moja iliyosababishwa na mpira wa faulo.

Takwimu nyingine ambazo timu hizo inafanana ni kila upande umefunga mabao 14 kupitia upande wa kulia.

Kwa upande wa Yanga, takwimu zinaonyesha imefunga mabao 35 yaliyotoka na kutengenezwa na viungo kupitia katikati ya uwanja ambapo inaonekana eneo hilo ni hatari zaidi, huku upande wa kushoto ukizaliwa magoli matatu pekee.

Yanga inaonekana hatari wachezaji wake wakiingia ndani ya boksi, kwa sababu takwimu zinaonyesha mabao yake 41 yamefungwa ndani ya eneo hilo, huku mengine 11 yakifungwa nje ya boksi.

Takwimu pia zinaonyesha mabingwa hao watetezi, Yanga imefunga mabao 28 wachezaji wake wakitumia mguu wa kulia, na ya mguu wa kushoto wakiwa ni magoli 20, manne yakiwa ya vichwa.

Yanga inayofundishwa na Kocha Mkuu Miguel Gamondi, haijafunga bao lolote kwa kona, lakini imefunga magoli mawili kwa penalti na mabao manane yamepatikana kwa njia ya krosi.

Kwa upande wa Wekundu wa Msimbazi, mabao yaliyopitia katikati ya uwanja, yakitengenezwa na viungo wake ni 22, ikiwa ni pungufu kwa watani zao, na kufunga mabao nanne kupitia upande wa kushoto, ikiizidi Yanga goli moja.

Imefunga mabao 35 ndani ya boksi, matano nje ya boksi, takwimu ambazo ni chini ya zile za Yanga.

INAENDELEA UKURASA 23

## Yanga yamalizana na Mzize 'kibabe'

**Na Saada Akida**

WAKATI Azam FC ikiwasilisha ofa 'nono' la kutaka huduma ya mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize, mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara wamemalizana na nyota wake kwa kumpa mkataba mpya, imefahamika.

Taarifa kutoka Yanga zinasema mshambuliaji huyo amesaini mkataba mpya wa miaka

INAENDELEA UKURASA 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >